

MLINZI, HABARI GANI ZA USIKU?



Asante sana, Ndugu Roy.

² Mnaweza kuketi. Nilikuwa tu nje nyuma ya pazia hapa, nikifurahia uimbaji huo mzuri. Je, mliufurahia huo? Huo ulikuwa mzuri kweli. Mungu awabariki hao watoto wadogo, wao ndio—ndio zao la kesho, kukiwapo na kesho.

³ Nami...Ndugu Rose alikuja na kunipeleka muda mfupi uliopita kwa dharura hospitalini, nami nikawazia, “Loo, hakika nitachelewa.” Bali sikuchelewa hata hivyo. Lakini aliniambia angechukua nafasi hiyo, kwa hiyo ninajua yeye ni hodari wa kufanya hivyo.

⁴ Vema, tuna furaha usiku wa leo kuona huku kukusanyika usiku huu wenye joto. Nasi tuna furaha kusikia taarifa kutoka kwenye mkutano wa jana usiku. Sijui kama kuna mtu yeyote hapa anayeweza kuonyesha, ama angeinua mkono wake, ambaye aliombewa na huduma hiyo mpya jana usiku anayeweza kuonyesha, anayeweza kujua kwamba kuna afueni dhahiri katika hali zao? Hebu tuone mkiinua mikono yenu, kwa wale waliopitia, waliopitia kwenye mstari wa maombi. Vema, sawa, hilo ni zuri. Vema.

⁵ Mtu fulani aliniambia ya kwamba yule mtu aliyepooza kwenye kiti cha magurudumu hapa jana usiku, ameketi huko nyuma mahali fulani katika kusanyiko usiku wa leo bila kiti cha magurudumu. Nasi tunafurahi kujua hilo. Uko wapi, ndugu? Waweza kuinua mkono wako, popote ulipo, yule ndugu aliyekuwa kwenye...Huyu *hapa*, ameketi papa *hapa*. Bwana ashukuriwe. Hilo—hilo ni sawa. Hiyo inaonyesha ni nini kuachilia imani ndogo ianze kutenda kazi.

⁶ Sasa, huduma mpya ni kulaani ugonjwa ulio mle ndani. Mmeona yale Roho Mtakatifu amefanya? Jambo la kwanza, aliponiambia, lilikuwa ni kuwaombea wagonjwa. Sasa, nililalamika, na kusema, “Hawataniisikiliza, kwa sababu mimi sina elimu.”

⁷ Naye akasema, “Kama Musa alivyopewa ishara mbili, utapewa mbili.” Halafu akasema, “Ya kwanza, watu wataweka tu mikono yao juu ya wako, nawe utawaambia, hata wataona athari yake, kama umetoweka ama la.” Sasa mnaona, hiyo inakuwa, inakubidi kuangalia hilo, hilo linakuwa burudani.

⁸ Halafu akasema, “Kama hawataiamini hiyo, basi kutakuwako na ishara nyingine, ambayo ulizaliwa nayo,

utaona ono, na kujua yale watu wamefanya, na yote kuwahusu, na kadhalika.”

⁹ Nikasema, “Hilo ndilo lililonileta hapa, nimeambiwa kwamba hilo halikuwa sahihi.” Ndipo akaniwekea Maandiko, na hilo lilitosha. Lakini nitamani siku hiyo ije.

¹⁰ Ni wangapi walio humu jengoni usiku wa leo wanaokumbuka nilipokuja Pwani ya Magharibi kwa mara ya kwanza, na loo, kote kusini, na—na nilikuwa tu na huduma hiyo moja ya kule kuwekea mikono? Mnaweza kukumbuka hilo? Hebu waangalie tu marafiki! Vema.

¹¹ Basi je, niliwaambia ya kwamba Bwana aliniambia ya kwamba kutakuwa na huduma nyingine (Mnakumbuka hiyo?), ambayo ingekuwa ni kuyatambua mawazo ya moyo, na kadhalika? Vema, hizo huduma zimefanya kazi kikamilifu kote ulimwenguni. Mnaona? Moja ilitumika siku yake, hiyo nyingine ikamalizia siku yake.

¹² Sasa, baadaye kidogo, kama nikipata nafasi, ninataka kuwaambia yaliyotukia hivi majuzi tu, kuletwa kwa huduma mpya ya kunena tu neno. Nayo inaleta... Inalirudisha moja kwa moja mkononi mwa watu tena, kama watakuja wakiwa na msimamo mzuri na kuamini, halina budi kutukia.

¹³ Ni wangapi wamesoma kitabu cha... katika hicho kitabu? Vema, kuna wachache hapa ambao wamesoma hadithi ya maisha yangu katika kile kitabu. Wakati ilipokuwa... Jinsi ambavyo Yeye aliniambia ya kwamba nilizaliwa kuwaombea wagonjwa. “Wafanye wakuamini, kisha uwe mwaminifu unapoomba, basi hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi.” Je, mumewahi kusikia hayo hapo kabla? Hakika, mumesikia.

¹⁴ Vema. Sasa, hiyo... Ndipo ishara hizi na miujiza ya kuonyesha yaliyopita, yajayo, na yale yangekuwako, na yale yamekuwapo, na yote kulihusu, ilikuwa ni thibitisho la Masihi anayekaribia. Na kuwaacha watu... Ilikuwa ni kuwaonyesha watu ya kwamba nilikuwa nimewaambia ukweli, kwamba niliitwa kuwaombea wagonjwa. Hilo ndilo wazo, kuwaombea wagonjwa. Sasa, huduma ya pili inaondoka, na ya tatu inaingia, kwa hiyo nina furaha sana juu yake.

¹⁵ Sasa, kesho asubuhi, Kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel, nadhani wamekitangaza, mahali kitakapokuwa. Natumaini nyote mtakuwapo, ningetaka kusikia baadhi ya uimbaji huo zaidi. Na kwa hiyo, tutatarajia wakati mzuri huko chini juu ya ninii, kikombe cha kahawa, na chochote walicho nacho, na mayai ya kukaanga, na yale yanayoambatana nayo. Halafu basi, nitakuwa nikizungumza, Bwana akipenda, kesho asubuhi kwenye hicho kiamshakinywa. Bwana akiruhusu, ninataka kuzungumza juu ya *Kuuendea Ushirika Kwa Kikombe*, na halafu, iwapo hayo ni mapenzi ya Bwana.

¹⁶ Ndipo kesho usiku, turudi hapa tena kwa ajili ya ibada nyingine ya uponyaji wa Kiungu, Bwana akipenda. Na ni kadi gani za maombi, ama chochote kile, sijui kile Bwana atakachofanya, ama anachofanya, kuna kadi za maombi zilizosambazwa, hivi hazipo alasiri ya leo? Nilidhani zilikuwako. Vema. Tutaona kile Bwana atakachotuongoza kufanya kuzihusu usiku wa leo, kama itakuwa ni upambanuzi, ama kuendelea na huduma iliyosalia, ama yale atakayotutaka tufanye. Lakini kila usiku tutakuwa tukiwaombea wagonjwa, na kumtumainia Mungu kuokoa nafsi.

¹⁷ Sasa, kabla hatujalikaribia Neno, kuna watu wengi wanaoweza—wanaoweza kuchukua Biblia, na kuvuta hiyo jalada namna *hiyo*, bali inahitaji Mungu kulifungua hilo Neno, mnaona, Mungu pekee. Si la kufasiriwa apendavyo mtu binafsi, lisome tu na uliamini.

¹⁸ Sasa kabla hatujalikaribia, tukilisoma, hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu tunapozungumza na Mwandishi wake kwa dakika moja. Ni nani aliye na haja maalum usiku wa leo? Wewe inua tu mkono wako, ukisema, “Mungu, nikumbuke usiku wa leo.” Mungu na atujalie hizo haja, angalieni tu mikono, siku hii kuu, hata hivyo ni watu wahitaji.

¹⁹ Ee Bwana wa thamani, Baba yetu mwenye rehema sana na wa Kiungu, uliyemfufua tena Bwana Yesu katika wafu, na umemwasilisha kwetu katika nguvu za kufufuka za Roho Mtakatifu, akiishi pamoja nasi usiku wa leo, akifanya kazi, akithibitisha Neno Lake, akionyesha mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, tupate kuwa na hakikisho lililobarikiwa kwamba Yeye yu hai wala hajafa, hatutumikii kanuni za imani, kanuni zilizokufa, hatutumikii miungu ya sanamu, wala miungu iliyokufa, lakini Mungu wetu yu hai milele, anaishi pamoja nasi.

²⁰ Loo, jinsi tunavyoshukuru kujua katika saa hii, wakati giza linapotanda juu ya dunia na giza kuu juu ya watu, jinsi ambavyo tunakushukuru kwamba tuna Mwamba huu mkuu wa wokovu, ile Nanga ya hakika ya nafsi! Hata tunajua, haitubidi kulibahatisha, Mungu wetu aliyetufanyia hizi ahadi yu hai, na hujionyesha Mwenyewe hai miongoni mwetu, tayari kujibu maombi yetu, na kufanya lolote tunalotaka mioyoni mwetu, kama likipatikana katika mapenzi Yake ya Kiungu na ahadi Zake.

²¹ Sasa, Bwana, tungeomba usiku wa leo, hasa, kwa ajili ya wale walio wagonjwa na wanaoteseka, na kwa ajili ya mtu huyo wa thamani na mpendwa ambaye ndiyo kwanza tumwombe kule hospitalini, akiwa mahututi. Lakini tulipomwekea mikono tuliona uhai ukianza kuingia ndani yake tena. Tunaamini kwa moyo wetu wote ya kwamba mtu huyo ataishi, kwa sababu Wewe umetufanyia ahadi. Nasi tumetoa huduma yetu, Bwana, bure

na kwa moyo wetu wote, katika imani tukiamini ya kwamba utatujalia haja yetu.

²² Sasa, Bwana, tungeomba usiku wa leo, ya kwamba Wewe ungemchukua Roho Mtakatifu, na kulichukua Neno, na kutuhudumia, sawasawa na haja zetu. Unajua mioyo yetu, na kile tunachohitaji, na hali yetu ya kimwili, tunapoinua mikono yetu kwa ajili ya mambo mbalimbali, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utatujibu. Basi, Bwana, wakumbuke wale wanaopata ahueni majumbani, na waliofungiwa, na wale wasioweza kuja.

²³ Kisha utubariki hapa pamoja, na ibada itakapokwisha nasi tuelekee makazini mwetu mbalimbali, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau, waliomwona akifanya jambo fulani baada ya kufufuka Kwake kama tu alivyofanya kabla hajasulubiwa, nao wakasema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

²⁴ Sasa, kuchukua muktadha kidogo usiku wa leo, hebu tuwaelekeze kwenye somo la Maandiko katika Biblia, katika kitabu cha Isaya. Hebu na tufungue Isaya, mlango wa 21 wa Isaya, na tusome kifungu cha 11 cha Isaya 21:

Ufunuo wa Duma. Mtu ananililia kutoka Seiri, Ee mlinzi, habari gani za usiku? Ee mlinzi, habari gani za usiku?

Mlinzi akasema, asubuhi inakuja, na usiku pia: mkitaka kuuliza, ulizeni: rudini, njoni.

²⁵ Hapana shaka ilikuwa ni siku ya kutisha, labda wenye joto, na kila kitu kilikuwa kimechanganyikiwa sana, na ilionekana kana kwamba hakuna kitu kilichokuwa kikienda sawa, jiji lote limefadhaika, kwa sababu onyo baada ya onyo lilitoka kwenye mnara, “Kuna adui anayekaribia!” Lakini huo mji ulikuwa umezama sana katika dhambi, hata wasingeisikia sauti ya mlinzi kwenye mnara.

²⁶ Ingawa alikuwa amesema, “Nimeona mavumbi kutoka kwenye magurudumu ya magari yao ya farasi, na katika mwanga wa jua, ninaona silaha zao zilizosuguliwa na panga zao zinazometameta.” Lakini hawangeamini hilo, kwa sababu walikuwa wamezama sana katika dhambi.

²⁷ Na wakati mahali fulani pamejisalimisha kwa dhambi namna hiyo hawataki kusikia kitu chochote kilicho na onyo au usumbufu wowote kwao. Lakini haidhuru, sauti ilikuja, onyo baada ya onyo.

²⁸ Basi jioni ilipoanza kukaribia, labda wale wanawali vijana walikuwa wakikutana huko nje kwenye kisima cha umma kwenye uwanja wa mji kuchota maji ya jioni. Jambo ambalo lilikuwa ni desturi siku hizo kwa wasichana kwenda kisimani, na kuchota maji yao, asubuhi na mapema na baadaye alasiri,

ambayo yangekuwa kwa matumizi ya mchana, halafu matumizi ya jioni na usiku, ya kupika na chochote walichopaswa kuyatumia kwake.

²⁹ Na wakati hawa wasichana fulani, mandhari mtaani ingekuwa, tungewaona wakija kutoka sehemu mbalimbali za mji, nao walipofika kule, tungenikia kicheko kidogo cha kichinichini, wakisema, “Je, ulisikia yale yule mlokole kwenye mnara aliyosema leo, akijaribu kututisha tuingie kwenye jambo fulani? Alikuwa akijaribu kutuonya juu ya adui anayekuja, wajua, akitwambia ya kwamba inatupasa kuanza kutubu, na kuvaa nguo za magunia, na majivu.”

³⁰ Nao wangesema, “Sasa, hatutavaa nguo za magunia na majivu, wala kutubu, kwa sababu hatuamini ujumbe wake. Tunaamini ya kwamba usiku wa leo tunapaswa kufanya karamu, nasi tunapaswa kuvaa nguo zetu za mtindo mpya zaidi. Basi mnafikiri kwamba tutamwacha mlokole asimame na kutwambia jinsi tunavyopaswa kuvaa na yale tunayopaswa kufanya? Sijali anapayuka kiasi gani, anaonya kiasi gani, ninaenda kwenye karamu haidhuru!”

³¹ Na kadiri ninavyochukia kulisema, hii ni siku fulani kama ile siku. Haidhuru utawaambia nini watu, wangali watafanya yale wanayotaka kufanya, wao ni wakaidi, nao wanaenda kutumbukia moja kwa moja. Haidhuru umeonya jinsi gani juu ya kuja kwa adui, ama kuja kwa Bwana, wataenda vile vile tu kama walivyofanya, wameamua. Ni wazimu wa raha, nao watafanya vile tu wanavyotaka kufanya. Na kama ukijaribu kuwasahihisha, wewe ni mlokole. Vivyo hivyo tu, sauti ingali inaita! Mungu atakuwa na mlinzi kwenye mnara Wake ambaye hatakosa kutoa onyo.

³² Kulikuwako na vijana katika—katika vilabu vya pombe, nao wangepishana vinywaji, na kusema, “Jim, ulisikia leo? Tuna adui anayekaribia.” Wakilidhihaki sana, na kufanya mizaha michafu. “Tunajua vizuri zaidi ya hayo, tuna mfumo bora zaidi wa kijeshi uliopo katika nchi hii, wala hakuna adui anayeweza kutusumbua, ngome zetu zote zimelindwa pamoja na kuta zetu. Na—na yule mlokole kule juu kwenye mnara, laiti wangemtoa mle!”

³³ Mwajua, kusema kweli miongoni mwa watu wanaotaka kuishia siku hizi hakupendwi na watu wengi, hawataki kuamini ukweli. Lakini Biblia ilisema, “Mtajua kweli.” Nina furaha sana kwa hilo! “Mtajua kweli, nayo kweli itawaweka huru.” Sasa, unaweza kuwa mfungwa, au, unaweza kuwa m—mfungwa anayekataa ukweli, au unaweza kujua ukweli na uwe huru.

³⁴ Ndipo usiku unapoanza kukaribia, basi ninaweza kuona hapa kwamba wakati vivuli vya jioni vilipoanza kushuka, na kazi za siku hiyo zilikuwa zimekwisha basi wote wakakusanyika mahali walipokuwa wanaenda kufanya karamu hii au mlo. Na

hayo yalikuwa tu karibu yote waliyovutiwa nayo. Na hayo ndiyo karibu yote ambayo watu wengi wanavutiwa nayo leo.

³⁵ Lakini ningewazia huyo mlinzi alipata kundi dogo ambalo lingemwamini na akatoka mle. Nina furaha sana usiku wa leo, kwamba tunao, bado, baadhi ya walinzi halisi ambao wanatayarisha kundi kutoka hapa moja ya siku hizi, maana shida inakuja, likijiandaa, kwa kuwa shida inakaribia, na walinzi waaminifu, wanaolinda urithi wa kondoo wa Mungu, wakiwaonya, “Jiwekeni tayari kwa ajili ya kukimbia, kwa kuwa utakuwa ni wakati ambapo hakuna atakayetoroka.”

³⁶ Kamwe hataweza kuepuka mabomu ya haidrojeni na oksijeni yatakapolipiga taifa hili. Kuna njia moja tu ya kuepukia, hiyo ni kutoka moja kwa moja mle, kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuwatoa, hicho ni nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo, kututoa kwake, pandeni juu, mwondoke msiweze kuyasikia, msiweze kuyaona.

³⁷ Basi wakati, labda mpira ulipoanza vizuri, nao wasichana wakaanza kucheza dansi pamoja na wanaume, na—na wanawake walioolewa na mume wa mwanamke mwingine, na vinginevyo, na vinywaji vikapitishwa, nao wote wakiwa na wa—wakati mzuri. Halafu basi, labda, labda mcheshi wa Hollywood, wa kisasa, ama mwigaji wa televisheni, akasimama na kuanza kufanya mizaha ya namna fulani kuhusu yule mtu kwenye mnara, “Je, ulisikia hilo leo?”

³⁸ Vema, wanasema tu jambo lilo hilo leo, hakuna tofauti. Ibilisi daima humchukua mtu wake, bali kamwe si roho, inaendelea kuishi juu ya mtu mwingine; Mungu humchukua mtu Wake, bali kamwe si roho, inashuka chini, ikiishi juu ya mtu mwingine. Kwa hiyo roho zile zile zingali ziko leo, sisi si vipofu kwa mambo haya. Na ingekuwa vema kama tungeisikiliza Sauti ya Yule aliye kwenye mnara, Roho Mtakatifu anayetuonya, “Ikimbieni ghadhabu ijayo. Iweni tayari, kwa maana saa inakaribia.”

³⁹ Na moja kwa moja katikati, kama ile karamu kubwa ya ulevi ya Mfalme Nebkadreza, tunaona wakati walipokuwa, wale waigaji walipokuwa wakiendelea na burudani yao, na watu wapendao anasa wasioyachukua maisha kwa uaminifu, kwa ghafla, walinzi walikatwakatwa langoni, ndipo wakaingia askari, askari wa mikuki, wa pinde, wa kombeo, wa mapanga, magari ya farasi yalikimbia juu ya mji, wakaingia kwenye bwalo la dansi. Nao hao wasichana wakabakwa, akina mama, waja wazito, walishindania jinsia ya mtoto ni ipi, nao wapasuliwa wangali hai, navyo vichwa vya watoto wachanga vikapasuliwa ukutani, nao wanaume wakauawa katikati yao, na yote yakaisha. Kwa sababu walishindwa kutambua na kupokea onyo la sauti ya mlinzi.

⁴⁰ Mungu alisema katika Biblia, “Liangalie lile kundi ambalo Roho Mtakatifu amekufanya mlinzi. Hakikisha ya kwamba

wamelishwa Chakula kizuri, wakijiandaa kwa ajili ya kuja kwa Bwana.”

⁴¹ Loo, jinsi ilivyokuwa huzuni wakati kilio hicho kikuu cha usiku wa manane kilipokuja na yote yakaisha! Inanikumbusha hadithi niliyosoma miaka kadhaa iliyopita kuhusu mtafuta madini huko Arizona. Alikuwa ni mmoja wa hao watu wasaka dhahabu, naye alitaka kuwa tajiri mara moja, kwa hiyo akaenda jangwani kutafuta madini. Alipokuwa akitafuta madini, hadithi inasema kwamba a—alipata kiota kikubwa cha vito vya thamani, na upesi tu akawa milionea na mwenye magunia yaliyojaa dhahabu.

⁴² Basi akambebesha maskini punda wake, naye, pamoja na punda wake, na mbwa wake mwaminifu wakaanza kurudi kwenye ustaarabu huku jasho likiruka kutoka usoni mwake, macho yake yakimetameta, na akienda zake apate kuwa na wakati mzuri maishani mwake mwote.

⁴³ Kwa hiyo, alipokuwa akikaribia mahali pake ambapo kikomo chake kingekuwa, kingekuwa, walisema kulikuwa na kibanda cha kale, kilichoachwa, basi akaingia kwenye kibanda hiki, na kuweka pesa mezani karibu na taa ndogo ya grisi, naye alikuwa akivikagua hivyo vibamba vya dhahabu, asijue ya kwamba macho yalikuwa yakimtazama. Basi mnamo wakati alipojilaza chini na kulala usingizi, mbona, alipoanza kulala, huyo maskini mbwa mwaminifu akaanza kubweka.

⁴⁴ Naye alikuwa amejilaza kwenye mto wake akitafakari, “Loo, kesho nitabadilisha vibamba hivi kwa fedha! Nami nitanunua magari makubwa, kisha nitakunywa wiski nzuri, nitafanya mambo haya yote, na niwe na wakati mzuri, na nitaenda kwenye kila dansi,” na yote ambayo angefanya, akiota ndoto hizo za mchana.

⁴⁵ Basi mbwa wake akaendelea kubweka, akibweka. Akaenda mlangoni, na kufungua mlango, na kusema, “Funga domo!” Ndipo mbwa akalia, alikuwa amefungwa kamba, naye akajaribu kumwonya bwana wake. Lakini akarudi tena na kujilaza kitandani mwake, na tena, mbwa akaanza kubweka tena.

⁴⁶ Naye akamwita mara kwa mara, “Funga domo! Sitaki kukusikia! Ninataka ndoto nzuri usiku wa leo ya nyakati nzuri nitakazokuwa nazo kesho nitakapouza dhahabu yangu.”

⁴⁷ Na hatimaye, mbwa akabweka tena, akakasirika, akanyosha mkono pembeni na kuchukua bunduki yenye mitutu miwili, akaenda mlangoni huku nyundo zote mbili zimevutwa nyuma, na kumpiga risasi yule mbwa akafa. Kasema, “Hiyo itakushughulikia. Sitakuhitaji tena, kwa vyovyote vile.” Akaiweka bunduki chini, na kujilaza kitandani, akakunja mikono yake pamoja na ndoto yake, akalala usingizi.

⁴⁸ Muda si muda, mlango ukafunguka kwa urahisi, mtu fulani akajipenyeza kupitia sakafuni, akachomeka ki—kisu cha kitara

kifuani mwake, akachukua hiyo dhahabu, akaondoka nayo. Loo, alifanya nini? Aliua ile sauti iliyokuwa ikimwonya! Hebu huo usiwe ndio msimamo wetu.

⁴⁹ Loo, ile Sauti ya Roho Mtakatifu inayolionya Kanisa, siku baada ya siku, tunapooni kuja kwa Bwana, hebu tusiitulize Sauti hiyo kwa kuipuuza na kuikataa, bali hebu na tutii onyo ambalo inatupa. Mungu ana walinzi juu ya urithi Wake.

⁵⁰ Ninaweza kukumbuka 1933, Agosti 16 saa nane alasiri, ninamaanisha Juni 16 saa nane alasiri. Nilikuwa ndio kwanza tu nimetawazwa kuwa mhudumu Mmishenari wa Kibaptisti, nami nilikuwa nikifanya uamsho wangu wa kwanza ambapo watu elfu tatu na kitu walihudhuria. Halafu basi, alasiri hiyo, nilikuwa nikiwabatiza waongofu mia tano u—ukingoni mwa mto chini ya Barabara ya Spring huko Jeffersonville, Indiana, mahali ninapoishi. Nao wapiga picha wa magazeti walikuwa huko nje, na wengi wa watu wa kanisa, kulikuwako na watu kama elfu saba ama elfu nane ufukoni.

⁵¹ Ndipo nikaingia majini, nao, kwaya ilikuwa ikiimba maskini ule wimbo mkuu wa Kanisa:

Kwenye kingo za Yordani zenye tufani
nasimama,
Na kutupa jicho tamanifu,
Kwenye nchi nzuri na yenye furaha ya
Kanaani,
Mahali ilipo mali yangu.

⁵² Yapata mtu wa kumi na saba au wa kumi na nane mashemasi na wadhamini waliyekuwa wakimwongoza majini alikuwa ni jamaa mdogo jina lake Colvin. Anga zote zilikuwa za shaba, mahindi yote yalikuwa yamenyauka, hatukuwa tumepata mvua kwa majuma matatu au zaidi. Loo, yalikuwa yakiteseka, mazao yalikuwa yanateseka. Na anga zilikuwa kama shaba.

⁵³ Ndipo nikamchukua jamaa huyu mdogo, nami nikamwambia, “Je, unamwamini Bwana Yesu, na umemkubali kama Mwokozi wako binafsi?”

Akasema, “Nimemkubali, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Nilikuona madhabahuni hivi majuzi usiku. Sasa, una hakika na jambo hili, kijana?”

Akasema, “Nina hakika.”

⁵⁴ Kwa hiyo basi, nikamshika mkono, na kuelekeza uso wake ukingoni, na kutangaza jina lake, na kumwomba Mungu ya kwamba atayabariki maisha yake. Nami nilikuwa tayari tu kumbatiza, wakati niliposikia Kitu fulani kikisema, “Angalia juu!”

⁵⁵ Vema, nikaogopa, nikafikiri mtu fulani ufukoni alikuwa akisema jambo hilo, nilikuwa tu mhubiri mvulana. Sikuwa

nimeoa bado, mke wangu mtarajiwa alikuwa akipiga picha ufukoni, ambaye ni mama wa mwanangu Billy.

⁵⁶ Ndipo nikaisikia tena, na mpaka mara ya tatu, kasema, “Angalia juu!” Ndipo nilipoangalia juu mbinguni, mahali yapata futi kumi mraba palionekana kama maji katika anga za samawati yakizunguka. Na kutoka kwenye mfano huo wa maji ya samawati, ikaja Nuru ikishuka kutoka Mbinguni. Watu wakaanza kupiga mayowe, wengi wakazimia.

⁵⁷ Nayo Sauti hiyo ikasema, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kuwaonya watu juu ya Kuja kwa kwanza kwa Kristo, huduma yako itawaonya juu ya Kuja mara ya pili, kote ulimwenguni.”

⁵⁸ Na mara baada ya hayo, bila shaka makala hayo yaliingia kwenye Associated Press hadi Canada, na kila mahali. Na imetimia. Kutoka kwenye huo uliohuishwa akaja Oral Roberts na wengine wote, basi uamsho umeenea kote ulimwenguni na ungali unaendelea.

⁵⁹ Kwa hiyo ninaona ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu, siku hizi, ndiye Mlinzi yeye yule aliyekuwa kwenye ule mnara hapo mwanzo, Yeye angali ni ile Sauti ya kuonya inayonena, “Jiweke tayari kukutana na Mungu wako.”

⁶⁰ Kila unapooni unywele wenye mvi, ni ishara huna budi kukutana na Mungu; kila unaposikia gari la kuchukulia wagonjwa likishuka kwenda mtaani, ni ishara huna budi kukutana na Mungu; kila unapopita makaburini, ni ishara huna budi kukutana na Mungu. Huna budi kukutana na Yeye wakati fulani ama mwingine, jiandae sasa, kwa maana saa inakaribia.

⁶¹ Mlinzi, nini, yeye, kazi ya mlinzi katika Agano la Kale ilikuwa nini? Mlinzi alikuwa ni mtu aliyepanda juu ya mnara juu ya mji, juu sana. Alikuwa juu kuliko askari wote wa miguu, kwa sababu palikuwa ni mahali pake. Sasa, ili mtu huyu aweze kufika kule juu, hana budi kuwa na ufahamu mzuri, dhahiri, na lazima awe na macho mazuri. Hana budi kuwa macho, hana budi kujua nyota, na sifa nyingi ilibidi ziwepo kabla hajaweza kuwa mlinzi sahihi.

⁶² Nami nahofu siku hizi, kwamba tumeweka baadhi ya walinzi mle ambao hawangeweza kuona mbali sana, loo, wasingeweza kuona maafa haya yote yanayokuja, wapate kuwaonya watu. Halafu, endapo hastahili, mlinzi angeuangamiza mji upesi, kwa sababu mji mzima ulimtegemea huyo mlinzi.

⁶³ Walinzi wa Mungu, kama tu ninii Wake... Katika Biblia manabii Wake walihesabiwa kuwa ni tai. Huyu tai, jinsi angeweza, angeweza kupanda juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote. Mwewe akijaribu kumfuata tai angesambaratika tu hewani. Asingeweza kamwe kufika kule, kwa sababu tai ni ndege aliyeumbwa maalum kwa kusudi hilo. Kama sivyo, alipopaa juu, manyoya yake yangemtoka. Je, uliwahi kujaribu

kuvuta manyoya kutoka kwenye bawa la tai? Loo, hayo ni manyoya makubwa, magumu, kwa sababu wanawabeba vifaranga wao kwenye manyoya haya, nao hawana budi kuwa juu sana. Nao wanaenda. . .

⁶⁴ Basi ingemfaa nini kupanda juu iwapo asingekuwa na uwezo wa kuona mbali sana? Hivyo ndivyo ninavyowazia siku hizi. Kama tukiwaelimisha wahudumu wetu, ina faida gani kuwaelimisha kama hawana ufahamu wa kiroho wa kuona mbali sana, kule kuja, na onyo la hatari? Ni kama tu kumpa kurumbizi wako vitamini nzuri atengeneze manyoya mazuri ya bawa, na kadhalika, halafu unamweka kwenye kizimba. Inafaa nini kumpa vitamini? Inafaa nini kujifunza juu ya Mungu *aliyekuwako*, kama Yeye si yule yule leo? Kuna faida gani kujifunza Biblia kama tutakana nguvu Zake zote? Lazima tufanyiwe maandalizi kwa ajili yake.

⁶⁵ Mtu huyu wa mnarani, alipanda juu, na basi kama jambo lolote lilitukia, alipaswa kuwaonya watu juu ya hatari yoyote inayokaribia. Tunamwona Bwana wetu Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuwa ndiye Mlinzi mkuu wa wakati huo. Nasi tunaona ya kwamba katika safari Yake ya duniani Yeye alinena zaidi juu ya Kuja Kwake mara ya pili kuliko alivyonena juu ya kuondoka Kwake. Alisema zaidi kuhusu Kuja Kwake mara ya pili, mara nyingi zaidi, kuliko alivyosema juu ya kuondoka Kwake. Moja kwa moja kwenye vivuli vya msalaba, Yeye aliendelea kunena juu ya Kuja Kwake mara ya pili, na kuwaonya watu kile ambacho kingetukia kabla tu ya Kuja Kwake mara ya pili. Yeye alikuwa Mlinzi, alikuwa Mkuu wa walinzi.

⁶⁶ Halafu basi, kama tukiona alishikilia hilo sana, kwenye vivuli tu vya msalaba, kupuuza jambo hilo na kunena juu ya Kuja Kwake, tunapaswa kuwa watu wa namna gani sasa tunapooona mambo hayo aliyonena yakitimia? kama lilikuwa kubwa sana hata kusulubiwa Kwake, na mateso Yake, na kila kitu kilimaanisha mengi sana kama lilivyokuwa, lakini, hata hivyo, Kuja Kwake mara ya pili kulikuwa zaidi sana, hata akapuuza kusulubiwa Kwake, na kuwaonya watu juu ya Kuja Kwake.

⁶⁷ Hebu na tusikie baadhi ya mambo aliyosema: Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu,” Yeye alisema, “kwa maana katika siku zilizotangulia ile gharika, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa, wala hawakujua, hata siku ile Nuhu alipoingia katika safina, ndipo ulimwengu wote ukaangamizwa.”

⁶⁸ “Hawakujua.” Kwa nini hawakujua hilo? Ni kwa sababu walishindwa kusikia sauti ya onyo la Nuhu, na kumwita mlokole, kwa sababu alikuwa na Ujumbe wa kweli wa Mungu, ilikuwa ni

ya kimbinguni. Mvua haikuwa imenysha kamwe, Mungu alitia maji mimea kote ardhini, lakini Nuhu akasema, “Mvua inakuja, na wote wasio katika safina hii wataangamia.” Alisimama mlangoni pa safina na kutangaza ujumbe wa maangamizi, ndipo akachekwa, na kudhihakiwa, na kufanyiwa mzaha.

⁶⁹ Leo hii Mjumbe wa kweli wa agano amesimama Mlangoni, ambapo Yesu ndiye Mlango wa wokovu, na Mlango pekee, na kudai ya kwamba Yeye ndiye njia pekee ya kuepukia, kabla tu ya hukumu.

⁷⁰ Nao watu waliosema... Kulikuwako na wenye kudhihaki siku hiyo, na kutakuwako na wenye kudhihaki katika siku hizi. Na jinsi walivyokuwa na kichaa cha anasa! Mnaona jinsi ulimwengu ulivyo siku hizi: una kichaa cha anasa. Alisema kutakuwako, bahari itanguruma, iangalieni siku hizi, mawimbi ya bahari, hayajasikika hapo kabla katika historia, haya hapa yakivunjika ufukoni na kuwaua watu. Matetemeko ya nchi mahali mahali, sina tu takwimu sahihi, lakini ninasahau ni kiasi gani matetemeko ya ardhi yamefikia ambapo kila saa *kadha*, kuna matetemeko *kadha* ya ardhi kote ulimwenguni, yakija tu wakati wote, kwa kuwa lile ganda dogo tunamoishi linazidi kuwa jembamba na jembamba wakati wote.

⁷¹ Nao watu wanaendelea kuishi moja kwa moja, wakisema, “Hakuna kitu kama kuzimu,” wanaangalia juu usoni pa Mungu, na kukana kuna kitu kama kuzimu, huku wameketi juu ya chungu chake. Volkeno zinazochemka, na dunia yote imetenguka, sayansi inasema dunia, huko nje baharini, inazidi kuwa na kina kifupi, kwenye Ncha ya Kaskazini inazidi kuwa na kina kirefu, kwa sababu dunia inapanuka. Loo, iko karibu tu kukombolewa. Na watu wanaona mambo haya...

⁷² Naye alisema kutakuwa na ghasia katika siku za mwisho, hakuna amani, hakuna utulivu. Angalieni siku hizi, kila taifa linaogopa hata kufa. Skrini za redio na televisheni zimewekwa kila mahali, mimi... za ninii, ninamaanisha, skrini za rada zimewekwa kila mahali, zikiangalia mahali fulani ili kombora liachiliwe. Basi kombora la kwanza litakapoachiliwa, itakuwa ni mlipuko kila mahali, kwa sababu kila taifa liko tayari. Mataifa haya madogo hayawezi kupuuzwa tena, kwa sababu yana kitu kile kile mataifa makubwa walicho nacho, na ni watu wasiomcha Mungu, na mataifa yasiyomcha Mungu. Basi itakuwaje?

⁷³ Ingekuwaje kama moja likiachiliwa kwa bahati mbaya? Likianza kuruka, lingepitia kwenye moja ya skrini hizo za rada, ndugu, wangeanza tu kuvuta wenzu, na makombora yangekuwa yakiruka. Je, mlisoma kitabu cha Tommy Hicks cha *Mwenendo Wa Wakati*, ambamo alikuwa na ile picha ya makombora hayo yote yametandazwa maili kadhaa, tayari, yameelekezwa kote duniani? Hayo mataifa mengine yana makombora yaliyowekwa, yameelekezwa kote duniani, na moja ya siku hizi jambo fulani

litatukia, nao wote watayaachilia wakati uo huo. Itakuwaje? Ulimwengu usingeweza kustahimili jambo hilo. “Mlinzi, habari gani za usiku?” Je, hiyo saa ni leo? Habari gani za usiku?

⁷⁴ Tunapona mambo haya yakitukia, loo, jinsi siku hizi tunavyohitaji uamsho, uamsho wa kuamshwa, lakini hatuwezi kuwa nao, kwa sababu saa hiyo imepitwa, mataifa yametenda dhambi yakamaliza siku yao ya neema. Siamini kamwe hatutakuwa na uamsho mkuu, wa ulimwengu mzima tena, utakuwa miongoni mwa Wayahudi, bali si kwa Mataifa tena, hakuna Andiko kwa ajili yake.

⁷⁵ Na mengi ya mambo mnyotazamia yaliahidiwa Wayahudi Kanisa likiisha kwenda Nyumbani, kwa hiyo tunakutazamia Kuja kwa Masihi wakati wowote. Hatujui ni wakati gani litatukia, bali inatupasa kuwa tayari na kuisikiliza Sauti ya maonyo. Loo, jinsi ninavyomshukuru Mungu kwa ajili ya wema Wake na ushirika Wake!

⁷⁶ Naam, vitu vya kutisha, bahari ikivuma, mioyo ya watu ikivunjika kwa hofu, mshangao wa nyakati, dhiki kati ya mataifa, mambo haya yote yalikuwa yatukie, nasi tunayo. Naye akasema, “Kanisa lingekuwa kaidi, lenye kujivuna, lipendalo anasa kuliko kumpenda Mungu,” angalia kote karibu nawe, “wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizua, na wasiowapenda walio wema. Wenye kudhihaki!” Loo, msikilizeni Roho Mtakatifu kutoka kwenye mnara wa utukufu usiku wa leo, akitangaza kwa nguvu angavu za ufufuo kwa moyo wa kila mwaminio. Iweni tayari, kwa maana saa imewadia. “Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu.”

⁷⁷ Sasa, tunafundisha sasa jinsi ulimwengu utakavyokuwa: amani hafifu, taifa dhidi ya taifa, ufalme dhidi ya ufalme, mambo haya yote yalikuwa yatendeke ulimwenguni, nasi tunayaona, watu wenye kichaa cha anasa, watu ambao hawakumpenda Mungu, waliopenda anasa kuliko Mungu, na hata hivyo wangukuwa na mfano wa utauwa, bali wangekana nguvu zake, hao nao mjepushe nao!

⁷⁸ Namna ya dini, tukijiita taifa la kidini, tukiwa na mfano wa utauwa, lakini tukikana nguvu zake. Nguvu zake zipi? Nguvu za Mungu! Nguvu za Mungu ni nini? Ni ufufuo wa Yesu Kristo, ambapo Mungu alimleta kutoka kaburini, na kumwasilisha Yeye, usiku wa leo, yu hai miongoni mwetu. Nguvu za Mungu, hakika.

⁷⁹ Sasa, Yeye aliliambia Kanisa, “Mtapata onyo: Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma—katika siku za Sodoma na Gomora, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

⁸⁰ Alisema kutakuwa na jambo fulani litakalotukia kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Mungu. Kama lilivyotukia kwa

Ibrahimu kule juu, na huko chini kwa Lutu, jinsi hao wahudumu walivyoshuka na kumhubiria Lutu toba, naye Lutu akajaribu kuwafanya watoto wake watubu, na wapendwa wake, nao wakamcheka na kumdhihaki.

⁸¹ “Sasa, Lutu, ulisema siku zote za miujiza zimepita, nawe hapa unakuja leo ukisema afadhali tukimbie mjini.” Walimcheka, kama mtu aliyekuwa akisimulia hadithi ya namna fulani.

⁸² Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Sikubaliani na Ndugu David aliposema ya kwamba kanisa la kawaida litapata uamsho tena. La, bwana. Wasingeuvumilia kamwe, la. Huenda ukaweka mhubiri kama rais katika kila jimbo katika taifa hili, nao watu wangukuwa wakaidi tu kadiri wanavyotaka kuwa. Hawataisikiliza hata kidogo. Huwezi . . .

Mama yangu alikuwa na methali ya kale ya kusini: Unaweza kumwongoza nyumbu kwenye maji, lakini huwezi kumfanya anywe. Mtu yeyote . . .

⁸³ Nyumbu, huyo ndiye mnyama mtovu wa heshima kuliko wote nimjuaye. Nyumbu ni kimoja tu cha vitu vikaidi sana na asiye na maarifa nilivyopata kuviona. Nawe unaweza kumwita, atasimama tu na kukukodolea macho, nawe useme, “Njoo hapa, jamani.” Naye atachomoza hayo masikio makubwa na kuangalia tu. Sema naye, na umwambie ukweli, atangojea apate nafasi, kama anakufa, ya kukupiga teke. Hiyo ni kweli. Ha—hana akili hata kidogo.

⁸⁴ Na hivyo ndivyo tu ilivyo na watu wengi siku hizi. Unaweza kuzungumza nao juu ya Kuja kwa Bwana, wanachomoa masikio yao na kukukodolea macho, bila kujua zaidi yale unayozungumzia kuliko nyumbu anavyojua. Hiyo ni kweli kabisa.

⁸⁵ Mnajua ni kwa nini nyumbu hawezi kuelewa? Yeye si ukoo safi. Mungu kamwe hakumwumba nyumbu, hilo lilikuwa ni kosa la mwanadamu. Mwanadamu aliwazalisha hao wawili pamoja. Nyumbu hawezi kuzaa tena na kumpata nyumbu mwingine. Inahitaji farasi jike, ama, na—na maskini punda kufanya *hivyo*. Wala hawezi kujizaa tena, amekwisha. Hajui ukoo wake, hajui ni wapi yeye. . . hajui baba yake na mama yake ni nani.

⁸⁶ Na hivyo ndivyo ilivyo na wengi wa watu hawa wanaojiita Wakristo siku hizi, wao si ukoo safi, hawajui maana yake, wao ni wafuasi wa kanisa fulani, bali hawajui baba na mama yao ni nani.

⁸⁷ Nitawaambia, ni tamu sana kuwa na farasi halisi, mzuri, wa ukoo safi, yeye ni mpole, mwema, anakuja na kukusugua, na kila kitu. Naye Mkristo halisi, wa ukoo safi, aliyezaliwa na Roho Mtakatifu, anajua wanachozungumzia. Wanajua Baba na Mama ni Nani, wanajua wamezaliwa na Roho Mtakatifu, wanajua la kufanya. Unaweza kuzungumza nao, wana akili ya kusikiliza.

⁸⁸ Huyo mwingine huchomoza masikio yake, akisema, “*Hoo, hoo!* Siku za miujiza zimepita. *Hoo, hoo!* Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.” Anaendelea kupaza sauti! Hiyo ni kweli. Lakini farasi anaelewa.

⁸⁹ Sasa, ni siku tunayoishi. “Na mlinzi, habari gani za usiku?” Alisema kutakuwa na wakati ambapo ingekuwa kama ilivyokuwa huko Sodom na Gomora.

⁹⁰ Sasa, Isaya hakuwa nje ya utaratibu, Isaya alikuwa katika utaratibu wa Mungu aliposema, “Usiku waja, na... Asubuhi inakuja, na usiku pia. Asubuhi inakuja, lakini usiku pia unakuja.” Sasa, sote tunajua hilo kwa—kwa jua kuondoka duniani linauacha mwezi ushughulike. Mwezi huangaza jua lisipokuwepo, kwa sababu nuru tunayotembelea ni nuru ya jua inayoakisiwa kutoka kwenye mwezi.

⁹¹ Sasa, hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kufanya: kuakisi Uwepo wa Mungu wakati Mwana ameondoka. Ndipo jua linapochomoza, mwezi umetoweka. Lakini kabla tu ya mapambazuko, hivi mliwahi kuona? Mwezi unapauka kabisa, nao unatoka. Nami nawaambia, kanisa tayari limepauka, lina upungufu wa damu. Liliondoka kwenye ile Damu, likaondoka kwenye wokovu, na Roho Mtakatifu, na mafundisho ya Neno, nalo limepungukiwa na damu.

⁹² Linashuka, basi ni jambo gani linalotukia? Jua linakaribia, nayo saa yenye giza kuliko zote ya usiku ni kabla tu ya mapambazuko. Sayansi inadai ni usiku, jua linakaribia, linasukuma, linakuja, na kusukuma, likiugandisha usiku pamoja, kwa sababu linajua lina muda kidogo tu halafu mchana utapambazuka. Na kabla tu ya mapambazuko, ni kitu gani kinachotokea? Nyota ya asubuhi. Nyota ya asubuhi inamaanisha nini? Anasimama peke yake, yeye ni mlinzi wa Mungu, anasimama kwenye mnara peke yake, nyota zingine zimefifia, mwezi umekwisha. Na kabla tu ya mapambazuko, jua linaanza kuangaza dhidi ya hiyo nyota ya asubuhi, nayo inaakisi nuru ya kweli ya jua la kweli ambalo karibu liko tayari kuangaza.

⁹³ Ni kitu gani? Ile Nyota ya asubuhi, Kanisa la Mungu aliye hai leo, Ambaye ni Mlinzi juu ya mnara akiwaonya mataifa na watu. Anasimama peke yake, mtu anayemtetea Mungu, husimama peke yake. Lakini Yeye anafanya nini? Yeye anaakisi Nuru ile ile ya Mwana iliyoshuka chini miaka mingi iliyopita, naye anafufuka tena.

⁹⁴ Huduma hiyo ya Kanisa la kweli ni ipi? Huduma ya Kanisa hilo itakuwa ni huduma ya Mwana, kwa sababu ni uakisi wa nguvu zile zile za Mwana, na Nuru ile ile ya Mwana, ambayo ulimwengu utajua wakati Mwana atakapofufuka, jinsi itakavyoonekana. Loo, kwa Kanisa leo, mtu atakayesimama kwenye mnara! “Mlinzi, habari gani za usiku?”

⁹⁵ Nyota ya asubuhi inaangaza, iko tayari kuakisi nuru ambayo jua linaiangazia nyota. Sasa, si hilo kanisa, si huyo mtu, jua ndilo linaloakisi kwenye nyota ambayo inaakisi nuru ya jua duniani. Sasa, si Kanisa, ni Roho Mtakatifu, kule kuja kwa Mwana wa Mungu ambako kunaakisi katika Kanisa ambalo linathibitisha nguvu Zake. Yeye anafanya jambo lile lile hasa, huduma ile ile aliyofanya wakati alipoondoka duniani, Yeye yupo hapa usiku wa leo akifanya jambo lile lile, akikuakisi Kuja Kwake! Kuakisi nini? Sio kupauka kwa mwezi, bali kuonyesha ishara zile zile. Ni kitu gani kinachotukia? Sio mwezi, nyota, nyota ya asubuhi inakutangulia kuja kwa jua.

⁹⁶ Loo, enyi nyota za asubuhi, inukeni mkaangaze! Ni wakati wa kuangaza, Kuja kwa Bwana kumekaribia. Ikiakisi Uwepo Wake, ikiakisi Mwana ajaye, ikitoa ishara zile zile, Yesu alisema iliakisi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, itakuwa vivyo hivyo katika kuja kwa Mwana wa Adamu.” Huduma ile ile ambayo Mwana alishukia, Nuru iyo hiyo aliyoshukia, inakuja tena katika nguvu za ufufuo, nayo Nyota ya Asubuhi inaakisi Nuru hiyo. Ndipo tunalia, “Mlinzi, habari gani za usiku?” Haleluya!

⁹⁷ “Asubuhi inakuja, na usiku pia.” Sasa tuko katika wakati wa giza, Wakati wa Kanisa la Laodikia, watu, vuguvugu, wasioweza kustahimili mambo ya Mungu, wanajiondoa, wakijitenga, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Lakini Nyota ya Asubuhi inaangaza moja kwa moja, vivyo hivyo tu, nguvu za Mungu, Roho Mtakatifu.

⁹⁸ Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya; kubwa kuliko hizi mtazifanya, maana Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Aliahidi nguvu. Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena,” itakuwa giza, “lakini ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari.” Ndipo Nuru ya Mungu itaakisiwa Kanisani Mwake, na kwa nguvu zaidi kuliko hapo awali, kabla tu ya kuja kwa Bwana Yesu. “Mlinzi, habari gani za usiku?”

Wakati Kuja kwa Bwana kunakaribia:

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;
“Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hayatapita kamwe!
Usitamani utajiri wa bure wa ulimwengu huu,
Ambao huharibika upesi sana,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hayatapita kamwe!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
 Ikiwa marafiki wa duniani wamekuacha,
 Bado shikilia karibu zaidi Naye!

⁹⁹ Tunaishi katika siku za mwisho. Ujumbe huu ambao Bwana alinipa mtoni niutumeme kote ulimwenguni, Yeye aliutangulia kwa kuuandika katika kila gazeti kwenye Associated Press: *Nuru Ya Ajabu Yatokea Juu Ya Mhudumu; Sauti Yanena Kutoka Kwenye Nuru*. Na sasa, kote ulimwenguni, ishara baada ya ishara, ajabu baada ya ajabu, haikosei hata wakati mmoja. Kikamilifu, maelfu, makumi ya maelfu, mamia ya maelfu limetendeka bila kushindwa hata mara moja, mahali popote. Ulimwengu wa kisayansi ulipiga picha Yake. Ni kitu gani? Ni Nguzo kubwa ya Moto. Nguzo gani ya Moto? Ile iliyowaongoza wana wa Israeli nyikani.

¹⁰⁰ Sasa, kama kitu chochote kina asili kitazaa asili yake ndani ya mtu huyo. Sasa, wakati Nguzo hii ya Moto ilipofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, wakati Mungu alipofanyika mwili katika Mwanawe, Kristo Yesu, sote tunajua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, sasa angalieni, wakati alipokuwa hapa duniani, angalieni huduma aliyokuwa nayo wakati alipozunguka.

¹⁰¹ Sasa, wao walisema, “Loo, unataka kuniambia ya kwamba Ibrahimu aliiona siku yako? Nawe, bado, hujapata umri wa miaka hamsini, nawe ulimwona Ibrahimu?”

¹⁰² Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” MIMI NIKO alikuwa ni nani? Alikuwa ni ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, iliyokuwa katika kijiti kilichowaka moto ikizungumza na Musa. Naam. “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.”

¹⁰³ Sasa angalieni kazi alizofanya. Sasa, Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari. Na kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.”

¹⁰⁴ Ulimwengu, kanisa, lile—lile *linalojiita* kanisa, pamoja na ulimwengu wa nje, hawataliona, wanasema, “Hakuna kitu hapo, usiamini upuuzi wa namna hiyo. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, hakuna kitu kama kunena kwa lugha, hakuna kitu kama karama za unabii, ati uponyaji huu wote wa Kiungu, huo ni upuuzi, siyvyo ulivyo.”

¹⁰⁵ Lakini Mungu aliahidi katika siku za mwisho ya kwamba angemwaga mvua ya masika na ya vuli juu ya Kanisa Lake. Siku za manabii, siku za mitume, Yeye angemwaga mvua ya masika na mvua ya vuli katika siku za mwisho, nasi tumeipata. Bwana yupo hapa, akionyesha yale hasa Yesu aliyosema yangetukia kabla ya kuja Kwake. Katika siku za mwisho, mambo haya yangetukia.

Sasa, tunajua jambo hilo, tunafahamu hilo, tunaishi katika saa hiyo ya kukaribia kwa Bwana, tunaona ishara Zake kila mahali.

¹⁰⁶ Naye Mungu, aliposhuka, alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu. . .

¹⁰⁷ Mnasema, “Vema, baada ya Yeye—Yeye kuwa hapa duniani?”

¹⁰⁸ Alisema, “Nilitoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu.” Ni wangapi wanaojua Yeye alisema hivyo? Hakika, alisema. Kasema, “Nimetoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu.”

¹⁰⁹ Baada ya kifo Chake, kuzikwa na kufufuka, Paulo alikuwa anaenda zake Dameski, ndipo Nuru kuu, Nguzo ya Moto, ikakutana naye barabarani, na kuyapofusha macho yake. Naye akaanguka chini, na akasikia Sauti ikisema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Akasema, “U nani wewe, Bwana?”

¹¹⁰ Akasema, “Mimi ni Yesu.” Amina. Nguzo ya Moto! Na hapa leo, si kwa sababu ilipigwa pamoja nami, si kwa sababu hata ilipigwa kwenye mimbara hii wakati mmoja, si kwa sababu ilipigwa, ama si kwa sababu ulimwengu wa kisayansi unajua jambo hilo, bali Kanisa linajua jambo hilo, ile Nguzo ya Moto iko pamoja na Kanisa siku hizi. Kama Hiyo ni Nguzo ile ile ya Moto basi itafanya kazi zile zile alizofanya alipokuwa hapa duniani. Na wakati alipokuwa hapa, Yeye alisema, “Sifanyi neno lolote mpaka ninii. . . Nitakapomwona Baba analitenda kwanza.” Je, hiyo ni kweli?

¹¹¹ Alimwambia Filipo mahali alipokuwa chini ya m—mtini, alimwambia Petro jina lake, alimwambia yule mwanamke kisimani dhambi zake, alinena mambo haya yote mbalimbali, yule mwanamke aligusa vazi Lake, Yeye alitambua ya kwamba alikuwa na imani na akamwambia ugonjwa wake ulikuwa umeponywa, Yesu yeye yule, Mungu yeye yule, kwa maonyesho ya kisayansi, tunayo hapa kwenye picha iliyotundikwa huko Washington, DC katika Ukumbi wa Sanaa wa Kidini, Picha pekee ya kisayansi iliyowahi kupigwa ya Kiumbe cha kimbinguni. Amina!

¹¹² Iko wapi? Miongoni mwa Wapentekoste. Inafanya nini? Ikionyesha Kanisa la Ibrahimu, hilo ndilo Kanisa inaloendea, hao wengine hawataipokea. Ni kitu gani? “Mlinzi, habari gani za usiku?” Kama Hiyo ni Nuru ile ile, italeta Maandiko yale yale, itatoa ishara zile zile, itatoa nguvu zile zile, ni Yesu Kristo yeye yule, yeye yule jana, leo, na hata milele. Nasi tunaiishi, nasi tunashangaa, “Mlinzi, habari gani za usiku?” Nyota ya Asubuhi inaangaza juu yetu.

¹¹³ Usijenge matumaini yako juu ya mambo ya ulimwengu huu, ondoeni nia zenu kwenye huu. . . Sema tu, “Vema, nitaamini nitafungua ukurasa mpya, na kwenda kujiunga na kanisa.”

¹¹⁴ Usifanye hivyo, wewe zaliwa mara ya pili. Sijali kinachotukia, unapoteza marafiki wangapi, jirani yako anasema nini juu yake. Mbona, watalisema, hata hivyo. Mtu yeyote ambaye... "Wote waishio maisha ya kitauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." Kwa hiyo usijali hilo, endelea tu, useme, "Mungu, nipe Roho Mtakatifu juu ya misingi *Yako*, jinsi *Wewe* unavyonitaka nimpate, mmwage juu yangu, nipe imani, ninataka imani. Ninataka kuamini katika uponyaji wa Kiungu, ninataka kuamini katika nguvu za Mungu." Naye atafanya hivyo.

¹¹⁵ Siku moja huko London, Uingereza nilikuwa na maskini askari wa Limey, alikuwa akinipeleka huku na huko, akinionyesha mambo mbalimbali, hayo mandhari tulipokuwa kule kwenye ziara. Ndipo basi tulipotoka kwenda kwenye uwanja fulani, kamwe sitasahau jambo hilo, huko Uingereza, Visiwa vya Uingereza, kila sehemu ndogo tu ya ardhi imechukuliwa, karibu yote, pamoja na nyumba, idadi yao ni kubwa sana, nami nikaona mahali pa kupendeza, loo, palikuwa na ploti nyingi sana humo, moja kwa moja chini katika mahali pazuri pa kijani kibichi, penye nyasi, na miti imesimama kuzunguka, ndipo nikasema, "Bwana, kwa nini watu hawajengi nyumba hapa?"

"Loo," akasema, "Kasisi Branham, wasingeweza, hakuna mtu, anayejenga nyumba kwenye uwanja huo."

Vema, nikasema, "Kwa nini?"

¹¹⁶ "Vema," akasema, "yapata miaka mia mbili iliyopita, kulikuwa na tauni kubwa katika nchi hii, ya homa nyeusi." Kisha kasema, "Watu walikufa kama nzi," kasema, "waliwajaza kwenye mikokoteni wakawakokota, kisha wakarudi na kuwaokota waliosalia, na kurudi. Nao hata hawakuwa na muda wa kuwazika, waliwaweka tu chini kwenye bonde hili, wakafanya ibada, na kuwafunika tu. Kisha wakaendelea, na kuendelea, na kuendelea, mpaka maelfu waliwekwa kwenye bonde hili na kuzikwa hapa." Kasema, "Wote walifunikwa, miili yao yote imekwisha, lakini homa hiyo ilikuwa kubwa sana," akasema, "hata hakuna Mwingereza angejenga nyumba kwenye uwanja ambapo kitu hicho kiliwahi kuwa."

¹¹⁷ Nikawazia, "Naam, ninyi ni waangalifu sana mahali mnapoweka maskini makao yenu ya duniani hapa, lakini inapofikia wokovu, utajenga nyumba yako juu ya namna yoyote ya maskini kanuni ya imani, ama chochote kile."

¹¹⁸ Kwa nini usininii...? Imekufa, na imekufa muda mrefu uliopita, "Wenye mfano wa utauwa, huku wakikana nguvu zake." Kwa nini usijenge matumaini yako juu ya mambo ya Milele? Hayatapita kamwe! Yajenge juu ya "Kristo, Mwamba imara, ninasimama; sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao." Jenga juu ya lile Jiwe lililo hai, si kitu kilichokufa na kutengwa

na Mungu miaka mingi iliyopita, jenga tumaini lako katika kitu fulani sasa, ambamo Mungu anaishi sasa.

¹¹⁹ Kama nilivyohubiri si muda mrefu uliopita, ninaamini mara ya mwisho hapa, juu ya kurudi kwa malkia wa Sheba, jinsi huko chini katika nchi hiyo kuu ambako alikuwa, mbona, alisema, “Mbona, miungu hawa wote tulio nao hapa chini, tunasikia habari zao, bali hakuna mmoja wao anayeishi, hawafanyi lolote. Tunasikia huko Israeli, wana Mungu huko juu anayeishi moja kwa moja ndani ya mwanadamu, naye ana upambanuzi wenye nguvu, unaoweza kujua mawazo ya moyo, hekima na nguvu za Mungu ziko pamoja naye. Na kama Mungu huyo ni bora kuliko mungu wetu, ninamtaka Mungu *huyo*, Yule aliye hai!”

¹²⁰ Hivyo ndivyo ilivyo kwangu usiku wa leo, ninamtaka Mungu ambaye ni Mungu aliye hai, wakati aliyo, sasa! Loo, nina furaha sana kwamba Yeye yu hai milele. Ninaona kukaribia Kwake, ninaona wakati ukitokea ambapo Yeye anakaribia kuja duniani, ninaona kila ishara ulimwenguni ikielekeza huko nyuma, kwamba katika mfumo wa ulimwengu, mataifa dhidi ya mataifa, jinsi ulimwengu unavyoenenda, jinsi wangekuwa na mfano wa utauwa, ninaona ulimwengu, ninaona mataifa, ninaona *linalojiita* kanisa, mfano wa utauwa, halafu ninaona Kanisa lililojazwa na Roho likiwa na ishara Yake inayoakisi kuja kwa Mwana, ile Nyota ya Asubuhi ikizima miale yake. Loo, jinsi nilivyo na furaha! Nina furaha kwamba Mungu ana Kanisa linaloweza kuizima hiyo miale; ni uakisi, acha Kristo ajiakisi Mwenyewe ndani yako.

¹²¹ Katika siku za kale walipotengeneza dhahabu, mpigaji aliipiga dhahabu hiyo na kutoa takataka, mpaka alipoona uakisi wake mwenyewe, ndipo akajua takataka zote zilikuwa zimetoka kwenye hiyo dhahabu. Wakati mwingine mnasema ninahubiri vikali sana, ninawararua watu. Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Utaiharibu huduma yako kwa kukemea mambo jinsi unavyofanya.” Kasema, “Acha mtu mwingine afanye hivyo.”

¹²² Nikasema, “Ni nani anayefanya hivyo?” Hiyo ni kweli. “Ni nani atakayefanya hivyo?” Kweli, nikasema, “Na—nataka kuninii...” Nikasema, “Ni... Mimi... Huenda ikawaumiza kidogo sasa, bali watanishukuru wakati huo utakapowadia.”

¹²³ Mtu anayehubiri chini ya uvuvio anawezaje kusema lolote isipokuwa lile Roho Mtakatifu analomwambia? Ile huduma ndogo ambayo Bwana amenipa, ninataka kuifanya iakisi Maisha ya Yesu Kristo kwa nguvu niwezavyo, ikifanya ishara Zake na maajabu yadhihirishwe. Naam. Furaha barabarani, ingawa inachosha.

¹²⁴ Ninakumbuka nilipokuwa mlinzi wa wanyama wa jimbo la Indiana, nilikuwa nikifanya doria kwenye nchi, kulikuwako na chemchemi ya kale huko chini sana Indiana ya kusini,

huko chini kwenye Green, uh, Mto Hindi. Nilikuwa napenda kunywa kwenye maskini chemchemi hiyo, sababu ya mimi kuipenda, ilikuwa na furaha sana wakati wote, ningepitia kwenye chemchemi hiyo, nayo *ingebubujika, bubujika, bubujika, bubujika, bubujika* tu.

¹²⁵ Nikawaza, “Una furaha sana, ni kitu gani kinachokufanya kuwa na furaha hivi?” Nikasema, “Unajua ni kwa nini? Ni kwa sababu, labda, su—sungura hupitia hapa na kunywa maji kutoka kwako, na hilo linakufanya kuwa na furaha.”

“La.” Kama angeweza kuzungumza, angesema, “La, la, hilo silo, Ndugu Branham.”

Ningesema, “Vema, labda ni kwa sababu ng’ombe wanakunywa maji kutoka kwako.”

“La, hilo silo linalonifanya nibubujike.”

¹²⁶ Ningesema, “Vema, labda ni kwa sababu ninakunywa maji kutoka kwako. Kila wakati ninapokuja hapa, majira ya baridi kali, majira ya kupukutika majani, majira ya kuchipua, majira ya kiangazi, daima *unabubujika, bubujika, bubujika, bubujika*, ukibubujisha tu maji matamu, baridi wakati wote.” Niseme, “Vema, ni kitu gani kinachokufanya ububujike basi?”

Angesema, “Si mimi ninayebubujika, ni kitu fulani nyuma yangu, kinachonisukuma, kikinifanya kububujika.”

¹²⁷ Na hivyo ndivyo lilivyo Kanisa lililozaliwa na Roho wa Mungu, ni *kitu fulani* nyuma yao, kinachomwakisi Yesu Kristo. Amina. Sio hao wanaobubujika, ni *kitu fulani* nyuma yao kinachowabubujisha, kikiwasukuma, kikiinua sifa tukufu kwa Jina Lake, hawaionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa kuwa ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aminiye. Amina. Ninampenda kwa moyo wangu wote. Mnampenda, vivyo hivyo?

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

¹²⁸ Baba wa Mbinguni, kwa kuwa siku inafikia sasa, ishara za kuonekana Kwake zimekaribia, tunalionga Kanisa, lile kundi dogo la wateule, walioitwa watoke, waliochaguliwa tangu zamani kabla ulimwengu haujaanza, majina yameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Roho Mtakatifu ametafuta kupitia katika mataifa na kote ulimwenguni, mpaka akaliita kundi hili dogo, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Wote wanijiao Mimi, ninampa Uzima wa milele, nitamfufua katika siku ya mwisho,” tunaona kundi hilo dogo likijikusanya pamoja kutoka katika kila dhehebu, kutoka katika kila kanisa, kutoka kila kijiji. Mungu akiliweka tayari kundi Lake dogo, akiacha Nyota ya Asubuhi iwaangazie, wanapokuona kukaribia kwa Bwana Yesu.

¹²⁹ Wakiona huduma ikitoka kwenye, “Mwenye haki ataishi kwa imani,” Martin Luther, utakaso kwa John Wesley, ubatizo wa

Roho Mtakatifu kwa Wapentekoste, na kurudishwa kwa karama, na sasa kuingia kwenye ile Nyota ya Asubuhi ipate kuanza kuakisi, nalo Kanisa lote linajiondoa katika kila kanisa, kila taifa, kila watu: Bibi-arusi kwa ajili ya Jina Lake.

¹³⁰ Ee Mungu, mioyo yao imejaa furaha, wana furaha. Wataketi katika majengo yenye joto, watatembea katika hali ya hewa baridi, watatembea kwenye mvua, mvua ya theluji, theluji, popote, “Kwa kuwa popote ulipo mzoga ndipo watakapokusanyika tai. Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu.”

¹³¹ Nami nina furaha sana, Bwana, kuhesabiwa pamoja nao, nina furaha sana usiku wa leo, kujua ya kwamba kuna Kanisa. Ulisema kungekuwako na Kanisa, lingekuwako bila waa wala kunyanzi. Baba, Ee Mungu, jalia majina yetu yawe kwenye kile Kitabu kikuu Huko juu, jalia tuonekane bila waa wala kunyanzi.

¹³² Isafishe mioyo yetu na dhambi, na hiyo ni kutokuamini, Bwana, tunatambua ya kwamba dhambi ni kutokuamini. Haidhuru tunaishi vipi, kama tungali hatuiamini Injili yote, sisi ni wenye dhambi kwa sababu sisi ni wasioamini. Jalia dhambi *zote* ziondolewe kwetu, Bwana, kutokuamini *kwote*. Nguvu za Mungu na zitulie katika kanisa hili usiku wa leo, kama vile Nyota ya Asubuhi, tunaomba, itakavyoshuka katika umbo la Roho Mtakatifu, na itaakisi huduma yenyewe ya Bwana wetu Yesu Kristo, ndipo wataona ni kwa nini walenzi ukutani wanapaza sauti, “Asubuhi inakuja!” Haleluya! “Asubuhi inakuja, na usiku umewadia, pia!”

¹³³ Ee Mungu, tunapoona kanisa likipoa, likifuatilia majengo makubwa, na madoido, na—na mambo ya ulimwengu, wakiwa na mfano wa utauwa, hawana nguvu, wakikana nguvu, wakiliacha, hata Kanisa la Kipentekoste linapoa, linafikia mahali ambapo furaha iko tu wakati muziki unapochezwa, Mungu, iko wapi mikutano ya maombi ya kukesha usiku kucha? Ziko wapi zile nyakati kuu za kupendana? Vipi...? Ni kitu gani kilichotukia, Bwana? Ninaomba ya kwamba Nyota ya Asubuhi itaakisi Nuru sana usiku wa leo, mpaka kila mtu hapa atauona Ufalme wa Mungu ukija katika nguvu, na kujua ya kwamba tunajiandaa kuingia katika jambo hilo. Tujalie, Bwana.

¹³⁴ Waokoe waliopotea. Bwana Mungu, kama kuna yeyote hapa usiku wa leo ambaye ni mali Yako, jalia waisikie Sauti Yako, jalia waisikie, Bwana. Huenda ikawa ni udhuru duni kwamba inatubidi kuimba wimbo, ama kulihubiri Neno, sauti zetu hazifai sana, lakini inakubidi kutumia sauti ya mwanadamu, kwa sababu huo ulikuwa ndio mpango Wako uliokusudiwa hapo mwanzo kunena. “Yeye awapokeaye ninyi anipokea Mimi, naye anipokeaye Mimi, anampokea Yeye aliyenipeleka.”

¹³⁵ Mungu, na iwe hivyo usiku wa leo, kwamba Mlinzi kwenye mnara, alipanda ngome za Utukufuni, ameketi mkono wa kuume wa Baba usiku wa leo, akifanya maombezi, jalia aje usiku

wa leo katika nguvu za kufufuka Kwake. Jalia aje miongoni mwetu usiku wa leo, na kufanya jambo lile lile alilofanya kabla hajasulubiwa, kusudi kundi hili dogo, la watu waaminifu, huku chini kabisa katika ulimwengu huu wenye dhambi, lipate kuona uakisi wa Yesu Kristo akidhihirishwa Kanisani. Nao wananinii. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . nguvu na utukufu, na tayari kwa ajili ya uhamisho unaokuja hivi karibuni. Tujalie, Baba. Tunalikabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Amina.

¹³⁶ Whiu! Loo, najisikia kubarikiwa, najisikia vizuri. Mnajisikia vizuri? Loo, kuna *kitu fulani* tu kinachonifanya nijisikie vizuri. Vema, mpiga piano, tupe sauti, *Nampenda*. Ni wangapi wanaompenda humu ndani? Inua mkono wako. Loo, vema, hilo ni sawa, ndugu. Sawa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹³⁷ Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, na kuuvumisha katika Roho. Sasa, Paulo alisema, “Nikiimba, ninaimba katika Roho; nikiabudu, ninaabudu katika Roho.” Sasa acheni tu kila kitu kiondoke, yule Roho Mtakatifu mzuri, Neno Lake, huisugua nafsi yetu. Ujumbe mkali wa kukemea umekwisha, ninii yetu. . . hatuna hukumu ya adhabu. Basi hebu tuinue tu mikono yetu tunapoimba.

Nampenda, (Mwabuduni tu.) Nampenda
Napenda. . . (Naam, Bwana, tunakupenda.)
Na. . . (Kwa moyo wangu wote, Bwana,
ninakupenda.)
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹³⁸ Loo, Yeye si ni wa ajabu? Yeye si ni mwema? Oral Roberts anasema, “Yeye ni Mungu mwema.” Yeye kweli ni mwema. Yeye ni Mungu mwema, halafu Yeye ni Mungu wa hasira, Yeye ni Mungu wa hukumu. Nina furaha sana kwamba kuna chemchemi iliyofunguliwa katika nyumba ya Mungu, usiku wa leo, kwa ajili ya usafi, wote walio wachafu wanaweza kuwa safi. Hivi hamna furaha kwa hilo? Nina furaha sana, nina furaha sana, ndugu zangu, dada zangu, nina furaha sana kwamba ndivyo ilivyo. Loo, jamani! Ninapenda tu kuhisi hisia ya namna hii.

¹³⁹ Ninakumbuka wakati mmoja nilipokuwa mvulana mdogo, kulikuwa na da—dada wa mhudumu fulani, nilikuwa na miadi naye, akasema, “Tutaenda wapi usiku wa leo, Billy?”

Nami nikasema, “Vema, hebu tutoke twende tukaendeshe gari huku, mahali fulani.”

Akasema, “Hebu twende tukaone sinema.”

Nikasema, “Siendi kuona sinema.”

Akasema, “Vema, kuna dansi huko chini kwenye Ukumbi wa Odd Fellows.”

Nikasema, “Siendi kwenye dansi.”

Akasema, “Sasa, ulisema hukuvuta sigara, hukunywa pombe, hukucheza dansi, huoni sinema.” Kasema, “Unapenda kujifurahisha na nini?”

“Loo,” nikasema, “ninapenda kuvua samaki, na kuwinda, na mambo kama hayo,” lakini hilo halikumpendeza.

Naye akasema, “Unapata wapi furaha yoyote?”

“Loo,” nikasema, “furaha ya Bwana ndiyo raha yangu.” Unaona?

¹⁴⁰ Basi siku chache usiku baada ya hapo, nilikuwa kwenye mkutano wa hema, akaanza...basi huyo msichana alikuwapo. Ndipo nikafanya wito wa madhabahuni, ndipo watu wakasukumana kwenye madhabahu hiyo, nikamwona ameketi kule nyuma akilia.

¹⁴¹ Nikasema, “Njoo hapa, Helen.” Naye akaja mahali nilipokuwa. Nikasema, “Unataka kujua ni furaha gani niliyo nayo?” Nikasema, “Hii ina thamani zaidi kwangu kuliko sinema zote na dansi zote,” nikasema, “ni furaha ya Bwana, ni amani ipitayo ufahamu. Ninajua ya kwamba siku moja nitakutana na watu hawa Utukufuni, wote wataokolewa na wawe Huko, na hiyo ndiyo furaha niliyo nayo.”

Akaushika mkono wangu, akasema, “Billy, hebu nipate furaha hiyo, pia.”

¹⁴² Nikasema, “Chukua tu mahali pako papa hapa. Haidhuru Elsworth alisema nini, simama papa hapa.” Na kulikuwa na vikuku mikononi mwake, na pete, na kadhalika, akainua mikono yake hewani, akaanza kupiga mayowe, na kupaza sauti, na kumsifu Mungu. Mungu akamwokoia na kumtakasa usiku huo.

¹⁴³ Na loo, najua ndugu yake alinijia, naye alikuwa tu akinikemea kuhusu hilo, kasema, “Ulimfanya dada yangu mlokole!”

¹⁴⁴ Naye akaja kwa miguu, tulikuwa tumesimama pembeni mwa barabara, akashuka kwenye gari, akaja pale akitembea, akasema, “Ninaliamini jinsi Billy anavyolihubiri.” Amina. Ile Injili ya mtindo wa kale, akasema, “Nina amani *hapa* ndani ambayo sijawahi kuwa nayo hapo awali, nami nimekuwa mshiriki wa kanisa tangu utotoni.” Mnaona?

¹⁴⁵ Loo, inakufanyia jambo fulani unapookoka *kweli*, *kweli* unapata *kitu fulani* moyoni mwako! Loo, maskini ule wimbo mdogo ambao Wapentekoste walikuwa wakiimba! Vema, siwezi kuimba, lakini hebu niujaribu:

Kuna watu karibu kila mahali,
 Ambao mioyo yao inawaka moto sana
 Kwa ule Moto ulioshuka kwenye Pentekoste,
 Uliowasafisha na kuwatakasa;
 Loo, unawaka sasa moyoni mwangu,
 Loo, utukufu kwa Jina Lake!
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao,

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao; (Haleluya!)
 Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Ingawa watu hawa huenda wasijifunze kuwa,
 Au kujivunia umaarufu wa ulimwenguni,
 Wote wameipokea Pentekoste yao,
 Kwa imani katika Jina la Yesu;
 Nao wanatangaza sasa, mbali na kwa mapana
 sasa
 Nguvu Zake zingali ni zile zile,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
 Mimi ni . . . kwamba ninaweza kusema mimi ni
 mmoja wao; (Haleluya!)
 Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Njoo, ndugu yangu, ukatafute baraka hii
 Itakayousafisha moyo wako na dhambi,
 Ambayo itapiga kengele za furaha
 Na itaiwasha moto nafsi yako;
 Loo, inawaka sasa moyoni mwangu,
 Loo, utukufu kwa Jina Lake,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Sote pamoja!

Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha kwamba ninaweza kusema mimi
 ni mmoja wao; (Haleluya!)
 Mmoja wao, mmoja wao,
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

¹⁴⁶ Hivi hamna furaha kulihusu? Nina furaha sana kwamba
 mimi ni mmoja wao. Sasa, peana tu mikono na mtu fulani

aliyeketi karibu nawe, useme, “Mimi ni mmoja wao.” Geuka tu, peana mikono, useme, “Mimi ni mmoja wao.” Haleluya!

Loo, mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao; (Haleluya!)

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana naweza kusema mimi ni
mmoja wao; (Haleluya!)

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

¹⁴⁷ Afadhali niwe Mkristo wa kale kuliko chochote nijuacho. Nina furaha sana kwamba Nyota ya Asubuhi inaangaza juu yetu, nina furaha sana ninatembea Nuruni kama vile Yeye alivyo Nuruni. Tuna ushirika sisi kwa sisi, na Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatusafisha na udhalimu wote. Nina furaha sana kuwa mmoja wao, sivyo?

Nikitazamia kuja kwa ile Siku njema ya ule
Utawala wa Miaka Elfu,
Wakati Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja
na kumnyakua Bibi-arusi Wake anayengojea;
Loo! moyo wangu unaugua, ukiililia siku hiyo
ya kufunguliwa kutamu,
Wakati Mwokozi wetu atakaporudi duniani
tena.

¹⁴⁸ Loo, nina furaha sana kwamba Yeye yuaja tena. “Nami nitamwona, nitamwona.” Kama vile watu wengine hawakuninii... Miaka mingi iliyopita kulikuwako na mwandishi, Fanny Crosby, alikuwa kipofu, hakuuza haki zake za mzaliwa wa kwanza, kama waimbaji wengi wazuri siku hizi katika ulimwengu wa televisheni na sinema, walivyouza haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa maskini nyimbo chache tu za bugi-wugi ama roki, lakini Bibi Crosby alikuwa ni mwanamke tofauti.

¹⁴⁹ Walimjia siku moja, na kusema, “Kwa nini usiandike ushairi wa kisasa? Kwa nini usiandike nyimbo ambazo zingeninii... kwa ajili ya ulimwengu wa burudani?”

Akasema, “Talanta zangu zote nilimpa Mungu.” Loo! Hmm!

Kasema, “Vema, unaamini kutakuwako na Mbinguni basi?”

Kasema, “Ndiyo.”

Kasema, “Nawe unafikiri utakuwa huko?”

“Ndiyo.”

Kasema, “Sasa, vipi, utakapofika kule, kama ukibaki kipofu,” kasema, “utamjua?”

¹⁵⁰ Akasema, “Nitagusa kovu la msumari mikononi Mwake.” Akageuka, akarudi nyuma, akirudi chumbani, ndipo alipofanya hivyo, akainua mikono yake na kuanza kumsifu Mungu. Walipotoka nje, yeye, wimbo ukamgusa, akasema:

Nitamjua, nitamjua,
Na huku nimekombolewa nitasimama karibu
Naye;
Nitamjua, nitamjua
Kwa alama za misumari mikononi Mwake.

¹⁵¹ Na leo hii, ndugu, dada, yeye anatembea kwenye barabara za Utukufuni akiwa na macho mazuri zaidi sana kuliko ambayo mtu yeyote humu duniani aliwahi kuwa nayo. Anamwona, anamjua, na amesimama karibu Naye, huku amekombolewa. Loo, kama ningemwuliza usiku wa leo, “Fanny Crosby, Kristo anamaanisha nini kwako?”

¹⁵² Angeniimbia wimbo huu, angeniimbia, kitu kama hiki, hebu tuone, mmoja wa nyimbo zake maarufu za kale nilizokuwa nikiziwazia muda mfupi uliopita, akasema, “Sina kitu katika ulimwengu huu, yote yako ndani Yake.” Ni wimbo gani huo sasa, ambao nilikuwa nikiuwazia dakika chache zilizopita, aliouimba? Huo ulikuwa ni wimbo mzuri sana, nilikuwa nikiimba-...Hata hivyo, ninakumbuka nikiuimba, nitaokumbuka katika dakika chache, ambamo alisema kwamba, “Yeye anamaanisha zaidi ya ulimwengu huu kwangu. Ni nani niliye naye duniani ila Wewe? Ni nani Mbinguni ila Wewe?”

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usinipite.
Wewe uliye Kijito cha faraja yangu yote,
Zaidi ya maisha kwangu,
Ni nani niliye naye duniani ila Wewe?
Au ni nani Mbinguni ila Wewe?

¹⁵³ Nina furaha sana kwamba hiyo ingeweza kumaanisha hivyo kwa mwanamke kipofu. Ingeweza kumaanisha nini kwako na kwangu, tunaoweza kufanya kazi, na kushughulika, na kumtumikia Bwana Yesu jinsi tunavyomtumikia. Mungu awabariki. Sasa...[Dada mmoja ananena kwa lugha, dada mwingine anafasiri—Mh.]

¹⁵⁴ Amina. Ndugu Fred, na Ndugu Norman, ndugu nilikuwa nimeketi nao asubuhi ya leo, kama hilo halikuwa jambo lile lile nililokuwa nikizungumzia asubuhi ya leo! Nilisema mavuno ya Marekani, wakati nilipoanza miaka mingi iliyopita, kwenye mavuno ya karama, na kadhalika, imeenea kote, imelichambua taifa, mavuno tayari yamevunwa, sasa tunarudi shambani

kupitia makapi, tukiokota punje moja hapa na pale, popote tuwezapo. Hiyo ni kweli, ndugu? Kisha kusema jambo lile lile hapa, Roho Mtakatifu anageuka moja kwa moja na kusema jambo lile lile usiku wa leo. Amina.

¹⁵⁵ Loo, Mungu hivi karibuni... Loo, kama wangeweza kufurahi wakati—wakati mavuno yanapoanza, tunapaswa kufanya nini sasa wakati mavuno yamekwisha? Wakati wa kupepetu emewadia sasa, kutenganisha makapi. Mnaona? Huu ndio wakati. Basi unawezaje kutulia bila kuyakemea vikali sana? Huu ni wakati wa kupepetu, naam, bwana, wakati u—unapopepetu ngano. Hiyo ni kweli kabisa. Huu ndio wakati unapokuja. Amina.

¹⁵⁶ Kama mtu yeyote hapa ambaye hana ujuzi wa Kipentekoste, naye anataka Roho Mtakatifu, hii *hapa* madhabahu, papa hapa sasa. Tutakuja papa hapa na kumwombea mtu yeyote ambaye hana Roho Mtakatifu. Mtu yeyote anayetaka kumpokea Yesu, ninakualika hapa madhabahuni.

¹⁵⁷ Kama umeona katika nyakati zilizopita, mimi sipendi sana kuwashawishi watu. Haininii... Ninajua ni vizuri, wakati mwingine watu wanarudi na kuzungumza mmoja na mwingine, lakini nimeona watu wakiongozwa mbali sana kutoka kwa Mungu kwa... Kama Roho Mtakatifu hatawainua kutoka kitini mwao, basi hawana matumaini, kwa vyovyote vile, kamwe hawadumu. Mnaona? Hiyo ni kweli. Kama kuhubiriwa kwa Neno...

¹⁵⁸ Ndipo Yesu akageuka na kumwambia yule mwanamke Msirofoinike, “Si vema Kwangu kukitwaa chakula cha watoto na kuwapa mbwa.”

Akasema, “Hiyo ni kweli, Bwana, hiyo ni kweli, lakini mbwa wako tayari kula makombo karibu na meza ya bwana wao.”

Akasema, “Kwa msemo huu, msemo huu...”

¹⁵⁹ Sasa, hili ni kanisa... Nataka mwone, jambo ni kwamba, hii huduma itaendelea kupanuka zaidi, mnaona, ka—karama ambazo Bwana ametoa ni kuthibitisha ya kwamba ninawaambia ukweli, ni thibitisho la Mungu kwamba ni kweli. Basi, ukweli ulikuwa ni nini? Nikasema, “Yeye alisema nilipaswa kuwaombea watu, nilizaliwa kwa kusudi hilo.” Nilisema hilo miaka mingi iliyopita.

¹⁶⁰ Karama hizi, ndio kwanza niweke tu huduma yote moja kwa moja kwenye karama. Mnaona? Nao watu, hasa Wamarekani, wanataka kuburudishwa. Walininii... Walifanya jambo lile lile na Bwana wetu. Lakini mara tu nilipoanza kusema kile nilichokuwa, kusema ukweli wangu, Mafundisho yangu ya Maandiko... Ambayo ningemwomba mtu yeyote anisahihishe katika hayo. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hakuna mtu ambaye hajawahi kufanya hivyo bado, nami ni mnyenyekevu tu, ninge kuwa tayari kulikubali wakati wowote.

¹⁶¹ Lakini mara Yesu alipoanza kuwaambia ukweli kuhusu Injili, ni nini kilitukia? Wale sabini wakaondoka, hao wengine wakaondoka, nao umaarufu wa Yesu uliendelea kushuka mpaka, hatimaye, wakamsulubisha.

¹⁶² Lakini huduma Yake iliendelea kuingia kilindi zaidi na zaidi, mara tu baada ya Yeye kufanya mkate huu, kama nilivyozungumzia usiku uliopita, na samaki, akageuka moja kwa moja na kuweka matundu, ma—macho ya mtu yasiyokuwa kitu ila matundu, akaweka mboni za macho, sasa, kulikuwako na umati uliofuata kwa sababu ya samaki na mikate tu, wanasema, “Tutaona atakalofanya kesho,” lakini mioyo yao ilikuwa mbali sana.

¹⁶³ Na katika wakati wa mwisho, alikuwa na wangapi wa kupanda juu kupokea baraka za Kipentekoste, kutoka katika makumi ya maelfu aliwahudumia? Mia moja na ishirini, kutoka kwenye makumi ya maelfu.

¹⁶⁴ Sasa, Roho huyo yuko ulimwenguni leo hii, akitenda huduma ile ile dhidi ya upinzani ule ule, itafanya jambo lile lile. Hiyo ni kweli. Lakini huduma Yake inazidi kuwa na kina zaidi na zaidi wakati wote, kuu zaidi.

¹⁶⁵ Sasa, sasa, kama hakuna mtu aliye tayari kuja, labda baada ya ibada ya kuwaombea wagonjwa, utakuja.

¹⁶⁶ Sasa, tuna... Billy yuko wapi? Ni kadi ngapi? Huh? Moja hadi mia moja? Moja hadi hamsini. Na ni herufi gani? A, A, moja hadi hamsini. Tulikuwa na zipi hivi majuzi usiku? Ninaamini tulianza na hamsini hivi majuzi usiku, sivyo? Hamsini? Vema, hebu tuseme, tuanzie mahali pengine, tulizichukua zote wakati huo. Hiyo ni kusema, nafikiri tulichukua chache kwa wakati mmoja, chache usiku mwingine mpaka tukazimaliza.

¹⁶⁷ Sasa hebu tuanzie mahali fulani kati ya moja na hamsini usiku wa leo, hebu tuanzie kwenye ishirini na tano. Tuanzie... Hapo ni katikati yao, ndipo tunaweza kuwagawanya vivyo hivyo. Vema? Hebu tuanzie... Vema, sababu ya mimi kufanya hivi, labda Bwana atatupa mstari wa upambanuzi, hebu tuone kinachotukia.

¹⁶⁸ Sasa, ni nani aliye na kadi ya maombi, ilikuwa ni nini? A? A, ishirini na tano, A, ishirini na tano. Mtu huyo hapo? Vema, njoo papa hapa. A, ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini. Hebu tuone, hiyo ni moja, mbili, tatu, nne. Vema. Thelathini na moja, thelathini na mbili, thelathini na tatu, thelathini na nne, thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini. Vema. Vema, sasa, tumefikia wapi sasa? A? A ilikuwa...? A, thelathini hadi arobaini. Vema, arobaini hadi hamsini, hebu wasimame, A, arobaini hadi hamsini. Hiyo ni arobaini na moja, arobaini na mbili, arobaini na tatu, arobaini

na nne, arobaini na tano, arobaini na sita, arobaini na saba, arobaini na nane, arobaini na tisa, hamsini. Hebu wasimame.

¹⁶⁹ Kama huwezi kusimama, inua tu mkono wako, tutamwomba mmoja wa mabawabu akulete moja kwa moja hapa kama wewe ni kiwete, ama chochote kile, ambapo tuliwaombea viwete na wanaoteseke hapa jana jioni.

¹⁷⁰ Nina furaha sana kukuona hapa nyuma bila kiti chako cha magurudumu usiku wa leo, ndugu. Nilisikia uliamka na kutoka nje jana usiku, ukisukuma maskini kiti cha magurudumu. Mungu awabariki. Hilo ni sawa. Mwanajeshi mstaafu, ninaamini, kutoka vitani, na—na jinsi Mungu alivyombariki, akaweka nguvu Zake na Roho juu yake, akatembea chini ya nguvu za Roho Mtakatifu, kiwete, amepooza, Naye Mungu akamfanyia mambo makuu.

Sasa, hebu tuone, je, ilikuwa moja hadi hamsini aliyosema? Nasi tukafikia hamsini, sawa.

¹⁷¹ Sasa, ni wangapi humu ndani wasio na kadi ya maombi, nawe unataka Mungu akuponye? Inua mkono wako. Hiyo haitakuwa hapa juu kwenye mstari wa maombi, ninii tu... Vema, wewe angalia huku, na uamini kwa moyo wako wote. Kumbukeni, Yeye angali ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Vema, kama ulimghusa Yeye, ungejuaje ulimghusa? Ingembidi kutenda vile vile alivyotenda.

¹⁷² Vema, ni wangapi kwenye mstari wa maombi huko nje, ambao hatufahamiani? Inueni mikono yenu, mnajua ya kwamba siwajui. Ninaamini ni kila mkono ninaoweza kuona. Ni wangapi huko nje ambao hatufahamiani, ambao siwajui? Inua mkono wako.

¹⁷³ Sasa, kama... Wengi wenu ni wagonjwa. Vipi kama—kama Bwana wetu Yesu, hebu tuchukue Andiko usiku wa leo, vipi kama Bwana wetu Yesu angekuja hapa, na alikuwa amevaa suti hii aliyonipa, nawe ungekuja hapa juu, na kusema, “Bwana Yesu, utaniponya?”

¹⁷⁴ Unajua kile Yeye angesema? Una wazo? Angesema, “Mtoto wangu, tayari nimefanya hivyo.” Ni wangapi wanaojua hilo?

¹⁷⁵ Kama wewe ni mwenye dhambi, kama ungesema, “Bwana, utaniokoa?” Tayari amefanya hivyo, inakubidi tu kulikubali. “*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*.” Hiyo ni kweli? Ni wakati uliopita. Sasa, lakini kama ulitaka kujua...

¹⁷⁶ Vipi kama mtu angesimama hapa amevaa joho refu jeupe, na nywele zikining’inia chini namna *hii*? Huenda ikawa hakuonekana hivyo. Hivyo ndivyo wasanii walivyoichora picha yake, Huenda alionekana tofauti kabisa na huyo kwa jumla. Lakini vipi kama angesimama hapa, na angekuwa na alama za

misumari mikononi mwake, alama za makovu katika paji la uso wake, na akasimama hapa na kusema alikuwa ni Bwana Yesu? Mwajua, upesi sana ningekwambia alikuwa amekosea. Hiyo ni kweli kabisa. Yesu atakapokuja, hapatakuwa na wakati baada ya haya. Hiyo ni kweli. Isingeweza kuwa ni Bwana Yesu.

¹⁷⁷ Lakini basi, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, angeweza kuwa hapa? Katika umbo la Roho Mtakatifu, ambapo Yeye alitutakasa, apate kuingia ndani yetu, na kufanya kazi Zake kupitia kwetu, maana hao ni mawakala Wake, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Hiyo ni kweli? Sasa, huenda akajitangaza Mwenyewe. . . Angejitangazaje Mwenyewe basi kujua ya kwamba alikuwa ni Yesu yeye yule? Kwa sababu ingekuwa. . . Yeye angeninii—Yeye angeweza kufanya kazi ile ile aliyofanya kabla ya kusulubiwa. Na hiyo ilikuwa kwamba Yeye—Yeye alifanya yale Baba aliyomwonyesha. Sasa, kama. . .

¹⁷⁸ Kuna mtu yeyote hapa ambaye hajawahi kuwa katika mmoja wa hiyo mikutano hapo kabla? Inua mkono wako. Hujawahi kuwa katika mmoja wa hiyo mikutano. Vema, Mungu awabariki, tuna furaha kuwa pamoja nanyi usiku wa leo.

¹⁷⁹ Sasa, ninyi huko nje, angalieni tu kuelekea Mbinguni, na kusema, “Bwana, mtu huyu hanijui, ninajua yeye hanijui, lakini mimi ni mgonjwa, sasa hebu nione kama ujumbe huo aliohubiri usiku wa leo, ‘Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma. . .’”

¹⁸⁰ Jinsi Malaika huyo alivyokuja pale, na kuketi chini kwa Ibrahimu, watatu. . . Malaika wawili pamoja na Mungu. Ni wangapi wanaojua huyo alikuwa ni Mungu? Ibrahimu alisema ilikuwa ni Mungu, alimwita Elohimu, Bwana Mungu. Anapaswa kujua, yeye ndiye aliyekuwa akizungumza Naye. Elohimu aliketi pale na nguo zilizojaa mavumbi, na kusema. . . Baada ya wale wahubiri wengine wawili kushuka kwenda Sodoma, Mmoja alikaa pamoja na Ibrahimu, sasa kumbukeni, Yeye alikuwa ni Mgeni, Naye akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

¹⁸¹ Alijuaje alikuwa ameo? Alijuaje alikuwa na mke, jina lake lilikuwa Ibrahimu, na jina la mke lilikuwa Sara? Nayo Biblia ilisema—ilisema ilikuwa hemani nyuma Yake.

Naye akasema, “Nitakuzuru kulingana na muhula wake, wakati wa uhai,” kama alivyoahidi. Naye Sara, akiwa ndani ya hema, akacheka kimoyomoyo.

Ndipo yule Malaika akasema, “Kwa nini Sara akacheka?”

¹⁸² Hiyo ni kweli? Hiyo ilikuwa telepathia ya namna gani? Sasa, Yesu alisema jambo lilo hilo litatukia kabla tu ulimwengu mzima haujateketezwa kama Sodoma na Gomora ilivyoteketezwa, Moto utashuka kutoka Mbinguni. Naye alisema jambo lilo hilo litatukia, kazi zile zile.

¹⁸³ Sasa angalieni, Martin Luther alikuwa wa kwanza katika yale matengenezo, alihubiri kuhesabiwa haki, kwa upana sana.

Ndipo akaja Wesley, ile Nguzo ya Moto ikasogea, Wesley, uh, Luther asingeweza kusogea kwa sababu alikuwa ameunda dhehebu, Nguzo ya Moto ikaondoka, Wesley akaifuata, utakaso, kazi ya pili ya neema. Alijenga kanisa kuu, akaokoa ulimwengu wakati huo, uamsho wa Kiwesley. Kitu gani? Wamethodisti? Mliunda madhehebu, mkamalizia fundisho lenu kwa nukta, “Tunaamini *hili* na si chochote kingine.”

¹⁸⁴ Wakati Roho Mtakatifu alipoanza kutoka tena, ile Nguzo ya Moto, Wapentekoste waliiona kama ubatizo, na ufufuo wa karama, Wawesley hawangeweza kuondoka kwenye hizo, Church of God, Pilgrim Holiness, Nazarayo, wasingeweza kufanya hivyo, walikuwa tayari wamekwamia kwenye utakaso. Lakini sasa ukaja ule ubatizo, Wapentekoste wakauona.

¹⁸⁵ Mlisikia yale Billy Graham aliyosema hivi majuzi? “Kanisa la Kipentekoste ndilo kanisa lenye nguvu sana linalokua kuliko yote yaliyopo ulimwenguni siku hizi.” Hiyo ni kweli.

¹⁸⁶ *Mgeni Wa Jumapili*, kanisa Katoliki lilisema hivi majuzi tu kwamba mwaka uliopita, ama ulikuwa mwaka ulioutangulia mwaka uliopita, ya kwamba Wapentekoste waliwaandikisha waongofu milioni moja na laki tano, kuliko kanisa lingine lolote lililokuwako ulimwenguni. Kwa nini? Watu ambao hata hawajui ABC zao, wakiihubiri Injili, nguvu za Mungu, hiyo ni kweli, Mungu aliahidi jambo hilo.

¹⁸⁷ Sasa angalieni, tunajiundia madhehebu sana, na kadhalika, “Nasi tuna *hili* tu. Naye anakuja juu ya farasi mweupe, si wingu jeupe, ama . . .” kadhalika, mpaka Roho Mtakatifu anaondoka moja kwa moja kutoka humo sasa, hiyo ni kweli, akitoka, na kulileta Kanisa, si katika mvua ya vuli, ama chochote kile, Yeye tayari yuko katika mvua ya vuli, Yeye analiumba tu Kanisa pamoja, kama tu ile piramidi kubwa huko chini Misri.

¹⁸⁸ Jiwe la kichwa kamwe halikuwekwa juu ya piramidi, kwa sababu jiwe la kichwa lilikataliwa. Hiyo ni kweli. Jiwe la pembeni lilikataliwa jengoni. Kwa hiyo, ni kitu gani? Kanisa, kila jiwe halina budi kujilundika na kujichonga, kama tu lile Jiwe la kuwekwa Juu, kusudi litakapokuja, litafanya Piramidi nzima, Mwili wa Kristo.

¹⁸⁹ Sasa, Roho wa Mungu katika Kanisa leo ni kama tu alivyokuwa wakati alipokuwa katika Kristo Yesu. Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Siwezi kufanya neno mpaka Baba Yangu anionyeshe. Baba anatenda kazi, nami natenda kazi hata sasa.”

¹⁹⁰ Sasa, kama Yeye atakuja usiku wa leo na kufanya jambo lile lile *huko* nje, *hapa* ndani, na kote, ni wangapi watakaomwamini Yeye kuwa ni Mwana wa Mungu aliyefufuka? Naye Mlinzi yuko ndani ya mnara, akionyesha ishara Zake na maajabu ya kule Kuja.

¹⁹¹ Njoo hapa, bwana. Sasa, huyu hapa mtu, ndio kwanza ainue mkono wake kwamba mimi na yeye hatufahamiani. Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu mwote, mpaka nilipomwona ameketi papo hapo muda mfupi tu uliopita, wakati alipoamka kuja huku. Simjui, sijawahi kumwona, Sijui yuko hapa kwa sababu gani, sijui lolote kumhusu. Sasa, sasa, kama ningeenda hapa, na kuweka mikono juu yake, niseme, ningesema, “Bwana, wewe ni mgonjwa?”

“Naam, bwana.”

¹⁹² Labda ndivyo alivyo, labda sivyo, sijui mimi. Lakini tuseme ndivyo alivyo, ninaweka mikono yangu juu yake, na kusema, “Yesu Kristo anakuponya. Nenda kwa amani.”

¹⁹³ Angeweza kuamini hilo, hilo ni la Kimaandiko, “Wataweka mikono juu ya wagonjwa.” Sasa, hivyo ndivyo Ndugu Roberts anavyowaombea watu. Vema.

¹⁹⁴ Sasa, mtu fulani aliniambia, “Ndugu Roberts atawaombea mia tano, huku wewe ukiwaombea hamsini.”

¹⁹⁵ Ninajua, mimi si Oral Roberts, Oral Roberts si mimi. Mnaona? Sote wawili tuna huduma zetu mbalimbali, Mungu huweka pamoja kutufanya Mwili mkamilifu, mnaona. Ndugu Roberts ni mtu wa Mungu, naye huwaombea wagonjwa, kadhalika na hao ndugu wengine, wote ni watu wa Mungu, nao wana njia mbalimbali za kuwaombea wagonjwa, hii ndiyo Bwana aliyonipa.

¹⁹⁶ Sasa, Yeye aliniambia niwaombee wagonjwa, niwaombee tu, niwawekee mikono, lakini akasema, “Ishara hizi, ishara hii utapewa, na hiyo ndiyo itakayowafanya watu kuamini.”

¹⁹⁷ Sasa, kama mimi ni kweli, ninasema kweli, ishara hiyo ni ishara ya Biblia, wote wanaojua hilo, iliahidiwa katika siku za mwisho. Sasa, nimezungumza habari zake, nimehubiri habari zake, nimezungumza habari zake, mmesikia habari zake. Sasa je, itafanya kazi? Jambo ndilo hilo. Kama hiyo ikifanya kazi, wao ni . . . kitu kingine chochote kitafanya kazi. Je, ilikufanyia kazi wakati Roho Mtakatifu alipokuja? Je, uliamini a—ahadi ya Roho Mtakatifu? Uliipata? Hiyo ni kweli. Ilifanya kazi vizuri. Unaona? Mungu hutimiza kila ahadi. Sasa Yeye hutimiza ahadi hii, sasa “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.”

¹⁹⁸ Sasa, huyu hapa mtu ambaye sijawahi kumwona, sijui lolote kumhusu, Mungu anajua hiyo ni kweli. Wala yeye hanijui, mimi simjui. Ni yeye tu anayenijua, kwamba ameniona, bali sijui lolote kukuhusu.

¹⁹⁹ Sasa, kama Roho Mtakatifu angali ni Roho Mtakatifu, nami ninaweza kujisalimisha kwa Roho Mtakatifu kwa karama ya Kiungu ya kujistarehesha tu, kama tu ilivyokubidi kufanya, kumpokea Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, na kadhalika,

ilikubidi kujistarehesha, kumwacha tu Yeye achukue mamlaka, sasa, kama ninaweza kujisarehesha, ili Yeye aweze kuingia na kuzungumza na mtu huyu, na kumwambia jambo fulani kumhusu, kile, anajua kama ni kweli ama si kweli, kile kilichokuwako, yeye atajua kama hiyo ni kweli ama si kweli. Vema, kama Mungu anajua yaliyokuwako, anaweza kujua yale yaliyokuwako, hakika, yeye angeamini yatakayokuwako basi, yale anayosema yatakuwako. Mnaona? Sasa, hilo linalifanya hakika.

²⁰⁰ Sasa, kama mtu yeyote ana shaka, unakaribishwa kuja hapa, kuchukua mahali pang'u, unaona, umekaribishwa.

²⁰¹ Sasa, sasa, nisingesema hilo bure, kama Yeye hakuwa amenipa ahadi hiyo. Na kote ulimwenguni mbele ya watu nusu milioni kwa wakati mmoja, nimemwona, wala hajashindwa kamwe, mbele ya wachawi, na kadhalika. Nami ninajua ya kwamba Yeye ni Mungu, kwa hiyo nina ujasiri.

²⁰² Sasa, kama Roho Mtakatifu angenena kupitia kwangu na kumwambia mtu huyu jambo fulani, ingewafanya ninyi nyote kuamini jambo hilo, ninyi, ninyi nyote muamini ya kwamba Yeye ni Roho Mtakatifu hapa?

²⁰³ Sasa, Baba wa Mbinguni, ninatambua ya kwamba ningekuwa bubu tu kama maikrofoni hii. Maikrofoni hii haiwezi kujinenea yenyewe, bali imetengenezwa kubeba sauti yangu. Bwana, nifanye, sasa hivi, kuibeba Sauti Yako, ile Sauti ambayo Wewe ungenena. Simjui mtu huyo, yeye hanijui, bali Wewe unamjua, na unanijua mimi, kwa hiyo nifanye tu, Bwana, kwa karama ya Kiungu iliyoamriwa kabla ulimwengu haujaanza, kwamba huduma hii inapaswa kuwa katika siku hii, kama tu vile huduma zote zilivyoamriwa kwa ajili yake... Mungu huweka kanisani mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti, na kadhalika, Mungu hufanya hivyo, hizo ni karama Zake zilizokusudiwa.

²⁰⁴ Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utawafanya watu waone. Ndipo kabla sijarudi kwenye mji huu tena, kama Wewe ukija, ama wengi wa hawa wakiendelea, basi Baba Mungu, kwenye Siku hiyo hakutakuwa na udhuru. Sasa, nimenena habari Zako, nena Bwana ya kwamba nimesema kweli. Ninajikabidhi Kwako pamoja na kusanyiko hili, nikichukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁰⁵ Sasa iweni tu na kicho, msiwe na shaka, aminini mambo yote. Sasa, neno moja tu, maana nimekuwa nikihubiri. Sikukusudia kulifanya hivi, nilikuwa tu nikienda kuwaombea wagonjwa, lakini nilipoona kundi la watu ambao hawakuwa wamehudhuria mikutano hapo awali, nilifikiri lingekuwa ni jambo zuri kama ningelifanya.

206 Ninazungumza nanyi kama tu vile Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani. Baba alimtuma huko juu, Yeye alijua alipanda juu kule, bali hakujua la kufanya. Huyu mwanamke akatoka, kwa hiyo akaanza kuzungumza naye, ndipo alipowasiliana na roho yake, aliona shida yake ilikuwa ni nini.

207 Sasa, kama Bwana Yesu yuko hapa . . . Roho yangu haikujui, sikujui wewe, sijawahi kukuona, lakini kama Bwana Yesu anakujua, na kama Roho Wake anaweza kuwasiliana nawe, kisha anitumie kuzungumza, anaweza kusema jambo lile lile, kama alivyomfanyia yule mwanamke pale, kwamba—kwamba ni nini.

208 Sasa, kama Bwana atanifunulia jambo fulani lililokuleta hapa, na bila shaka, tunajua una uzito kupita kiasi, lakini jambo fulani mbali na hilo, unaona, hilo lingekuwa . . . ingekufanya uamini? Ingekuwa . . . ikupe imani katika Mungu kukufanya uamini? Nalo kusanyiko lilisema lingewafanya waamini. Sasa, Bwana na alijalie.

209 Sasa, kama kusanyiko bado linaweza kuisikia sauti yangu, ninamwona mtu huyo akirudi nyuma, naam, ana ngiri, ana ngiri inayomsumbua. Hiyo ni kweli.

Unaamini? Sasa, nisingeweza kuiona hiyo, bali yeye anayo.

Unasema, “Huenda ulibahatisha, Ndugu Branham.”

210 Hebu kidogo, tutaona kama ndivyo ilivyo. Ninaamini, nitajaribu kuweka hilo niani mwangu, niliona henia, ama *chochote kile*, ngiri, ninaamini ilikuwa, ngiri. Nawe una ugonjwa wa moyo, pia. Umekuwa na—umekuwa na ajali ya motokaa, pia, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Nawe hutoki hapa, la, bwana, unatoka kwenye mji unaoitwa San Francisco, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Yesu Kristo anakuponya, rudi ukishangilia. Imani yako imekuokoa.

211 “Kama utaamini tu!” Sasa iweni na kicho kabisa, mnaona. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . amini. Siwalaumu, Bwana asifiwe, hakika, Mungu ni kitu cha kuabudiwa, hakika. Ninamaanisha kaeni tu vitini mwenu, iweni na imani. Usi—usishuku hata kidogo, amini tu kwa moyo wako wote. Sasa, baadhi yenu huko nje anzeni kuomba, mkiamini, inamisheni tu vichwa vyenu, na uinamishe moyo wako, badala ya kichwa chako.

212 Sasa, mtu huyu hapa ni mgeni kwangu, ninaamini uliinua mkono wako kule chini ya kwamba hatufahamiani. Basi sikujui, sijawahi kukuona, na Mungu anakujua, sikujui. Sasa, kama Yeye ataniambia shida yako, ama jambo fulani ambalo umefanya, ama jambo fulani utakalofanya, ama jambo fulani unalopanga kufanya, ama kitu fulani tu unachojua kwamba sijui *chochote* kukihusu, ingeongeza imani yako, bwana?

Je, ingefanya hivyo kwa kusanyiko? Vema.

²¹³ Sasa, hawa hapa wanaume wawili ambao hawajawahi kukutana, hawajawahi kukutana hapo awali maishani. Sasa, hii ni sawa tu na wakati Simoni Petro alipomjia Bwana Yesu. Na jina lake lilikuwa Simoni, kwa hiyo akamwambia jina lake lilikuwa ni Simoni, kasema, “Wewe ni mwana wa Yona.” Naye alipokwisha kumwambia, akazungumza naye, Petro aliamini. Sasa, Bwana Mungu anamjua mtu huyu, simjui. Lakini kama Bwana atafunua jambo fulani, alisema ingekufanya uamini, kuwa na imani, ulisema ingekufanya uamini. Sasa, Bwana na alijalie, wakati tu ninapojinyenyekeza.

²¹⁴ Sasa, rafiki yangu wa thamani, tuko hapa katika Uwepo wa Mungu, tuko hapa si kwa kusudi lingine ila utukufu wa Mungu. Sasa, kama utakuwa tu na imani, wala usitie shaka, na kuamini! Naam, unaugua ugonjwa fulani kama vile fistula ya rektamu, hiyo ndiyo shida yako, fistula, hiyo ndiyo unayotaka uponywe. Kuna jambo la kigeni kwako, wewe ni mhubiri. Hiyo ni kweli. Nami ninakuona, ulikuwa ukihubiri papa hapa. Lakini huninii. . . wewe hauko hapa sasa, uko karibu na m—mji unaoitwa Eureka, kitu kama hicho. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Wewe ni Kasisi Howard Call, BWANA ASEMA HIVI. Amini. Mungu akubariki.

Unaamini kwa moyo wako wote? Amini tu, hilo tu ndilo unalopaswa kufanya. Mwamini Mungu, usiwe na shaka.

Sasa, mama, sasa, unaona, sasa hivi angalia hapa mkononi mwangu. Unaona? Umeninii tu. . .

²¹⁵ Mama aliyeketi hapo akiugua ugonjwa wa mapindi, anasumbuliwa, akimwomba pia dada fulani, naye dada huyo yuko katika hospitali ya serikali. Lakini uligusa upindo wa vazi Lake basi. Uligusa nini, mama? Vazi lake, Kuhani Mkuu. Sasa, mambo hayo ni kweli. Sasa kama ndivyo ilivyo, inua mkono wako ukitaka kulikubali. Vema. Mungu akubariki.

²¹⁶ Haya basi, mnaona, mwanamke aliyeketi pale hata hayuko kwenye mstari wa maombi. Alifanya nini? Aligusa upindo wa vazi la Kuhani Mkuu, hilo latosha. Mwaminini Mungu sasa, keti tu na uombe kama yeye alivyokuwa.

²¹⁷ Sasa, hatufahamiani, sikujui. Sina njia ya kukujua, sisi ni watu wawili tu ambao wamekutana hapa duniani, mwanamume na mwanamke, kama, kama tu ilivyokuwa katika siku za Bwana wetu wakati kile kisima kidogo, walipokutana na yule mwanamke huko Samaria. Sasa, kama Bwana atanifunulia jambo fulani ambalo unajua sijui lolote kulihusu, basi litakufanya uamini, sivyo? Vema, Bwana na atujalie.

²¹⁸ Sasa, wewe ni dhaifu sana kwa sababu fulani, umefanyiwa upasuaji. Na upasuaji huo ulikuwa ni ugonjwa wa kansa, huo ulikuwa kwenye tezi, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa amini kwa moyo wako wote.

219 Shetani, ninalaani hali hii ya dada yangu, toka kwake katika Jina la Yesu Kristo!

220 Nenda ukapate afya sasa, kote. Nenda ukamsifu Mungu.

221 U hali gani, ewe msichana? Sikujui, hatufahamiani, bali Mungu anatumia sote wawili.

222 Sasa, hebu kidogo, mtu fulani, mtu fulani humu jengoni, kulikuwa na mwanamke mwingine aliyesimama hapa wakati huo. Unaona? Sasa iweni na kicho kabisa.

223 Loo, si ni ajabu kuwa katika Uwepo Wake? Marafiki, mnaweza kuamka kutambua ukweli kwamba Neno la Mungu limedhihirishwa? Sasa iweni na imani, ni mtu fulani hapa.

224 Sasa, kwenu tena. Mimi, kama ningeweza kukusaidia kwa njia yoyote, ningefanya hivyo. Lakini siwezi kukusaidia, ila... Kama Yesu angekuwa amesimama hapa, asingeweza kukusaidia, ingekubidi kuwa na imani katika Yake, yale ambayo tayari amefanya, kwa sababu mpango wote wa wokovu, kila baraka ya ukombozi, ilikamilishwa pale Kalvari wakati alipokufa. Unaamini hilo? Naam. Wewe ni Mkristo, ninaweza kuhisi roho yako, kwamba wewe ni Mkristo. Lakini husimami hapa kwa ajili yako mwenyewe, ni kwa ajili ya mtu mwingine, huyo ni mume wako. Hayupo hapa, ni mgonjwa, nyumbani, anasumbuliwa na kitu kinachomlemaza, ni yabisi kavu, ana ugonjwa wa ngozi. Mtu huyo alikuwa ni Mkristo, amerudi nyuma sasa.

225 Una binti hapa pamoja nawe, ana ugonjwa wa figo. Na—nanyi mna matatizo ya kinyumbani katika nyumba zenu, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI! Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini kwa moyo wako wote, na mambo haya yatasahihishwa? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaupokee. Amina.

226 Ninakupa changamoto kuamini kwamba ni kweli. Sasa, maono tu namna hiyo, sasa kusanyiko lote ni, nimekuwa katika mkutano baada ya mkutano, mpaka kusanyiko lote linaonekana kama, linaonekana tu angavu kwa namna fulani, kama mng'ao, kimulimuli juu ya kusanyiko hili, sasa hivi, huo ni Uwepo wa Roho Mtakatifu. Mnaona? Ninafikia mahali kama hapo sasa! Basi unaona, umeingia katika ulimwengu mwingine, kiwango kingine, milki nyingine. Nami ni—mimi ni dhaifu kama kwamba nilikuwa nimehubri tangu aduhuri ya leo. Hiyo ni kweli. Inanibidi kusimama kidogo tu, kwa sababu kwa namna fulani unajipumzisha mwenyewe. Sasa, hii ni ninii kadhaa, hii... .

Vema, tunamwambia mwanamke huyu hapa: Hatufahamiani, lakini Yesu anatumia sote wawili. Unaamini hilo? Vema, wewe amini.

227 Sasa, wakati Musa aliposhuka kwenda Misri kufanya ishara, kuwaonyesha watu ya kwamba Mungu alikuwa amemtuma, ishara hiyo ilikuwa ni thibitisho ya kwamba Yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Hiyo ni kweli? Alikuwa akiwaambia

ukweli, jinsi ya kuepuka ghadhabu ya taifa hilo, ghadhabu ya Mungu ilikuwa ikija juu ya taifa, ilibidi Pasaka ifanyike. Na sasa, Musa alishuka akaenda kule, na kufanya ishara ambayo Mungu alimwambia afanye, kugeuza kijiti kuwa nyoka na halafu anakiokota tena, na kufanya ishara yake kwa mkono wenye ukoma, nao Israeli wote wakamwamini bila mnong'ono hata mmoja, mnaona, walimwamini.

²²⁸ Lakini sijui ni kwa nini siku hizi watu hawaninii, wakati Yesu alisema jambo hili lingetukia, Huyu hapa, papa hapa usiku wa leo. Si—sikuwa na chaguo katika hili, mambo hayo yalikusudiwa tangu zamani na Mungu. Mnaamini hilo? Hakika, mnaamini. Yalikusudiwa na Mungu, mwanadamu hawezi kujifanya mwenyewe. “Ni nani akijisumbua aweza kujiongezea kimo chake hata mkono mmoja?” Lakini hii si njia rahisi, ni njia ngumu, mateso, mateso yasiyojulikana. Huwezi kuuambia umma, wasingeelewa hilo; huwezi kulielezea, kwa sababu wewe mwenyewe hulijui; inakubidi tu kuendelea na kufanya huduma yako, wakati yote yatakapokwisha unaenda nyumbani.

²²⁹ Sasa, ninazungumza nawe kama tu Bwana wetu alizungumza na yule mwanamke kisimani, kupata shida yako, nitaipata kwa neema Yake. Una TB, hiyo ni kweli. Pia una ugonjwa wa kansa. Una ugonjwa wa damu ambao madaktari hawawezi kufanya lolote kuuhusu, hauwezi kutibiwa. Hiyo ni kweli kabisa. Ninamwona, kwa namna fulani da—daktari mnene, anatikisa kichwa chake anapokiangualia kitu hicho, kasema, “Hakiwezi kufanyiwa chochote.” Hiyo ni kweli, hiyo inamwelezea. Sasa, ningejua je mle, moja kwa moja chumbani, kwenye maabara, mahali alipokuwa amesimama? Unaona? Sasa, una matatizo mengi ya mambo, mambo mengine yanayokusumbua, wewe ni mgonjwa kweli.

²³⁰ Wewe hutoki kwenye mji huu, la, unatoka kwenye mji mkubwa kuliko huu, na mji huo uko mashariki mwa hapa, ni Salt Lake City. Hiyo ni kweli. Kama Mungu ataniambia wewe ni nani, na wewe kote kutoka huko, kama Mungu ataniambia wewe ni nani, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Utaamini? Vema, Bi. Harvey, unaweza kurudi nyumbani, ukaponywe, Yesu Kristo anakuponya.

Unamwamini Bwana?

²³¹ Vema, njoo. Sasa, mtu anayefikiri kwamba unaninii, ya kwamba huenda unasoma mawazo yake: Njoo hapa, mama. Weka mkono wako juu ya wangu. Mungu ataniambia una shida gani, unaliamini? Ugonjwa wako wa moyo umeponywa. Nenda zako nyumbani, uwe mzima.

Sasa, na hilo je?

²³² Njoo, mama. Sasa, mwanamke huyu alikuwa na jambo lile lile, kwa sababu kuna nuru iliyotoka kwa mwanamke huyu

kwenda kwa yule. Endelea tu kusonga mbele, umeponywa, pia, Yesu Kristo anakuponya. Mungu akubariki.

²³³ Njoo huku, yeyote yule, chini kule, njoo *huku*. Sasa, kama Mungu ataniambia shida yako ni nini kwa kuangalia *huku*, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Shida ya mgongo. Nenda zako na ushangilie, useme, “Yesu ananiponya.” Amini kwa moyo wako wote, mwamini Mungu.

²³⁴ Sasa, unapoamka asubuhi, umekakamaa sana, pia, yabisi kavu ndiyo unayotaka kuombewa. Sasa, kama utamwamini Bwana kwa moyo wako wote, kesho usiku unaweza kukimbia kwenye kipandio hicho. Nenda uamini sasa, panda kipandio. Amini kwa moyo wako wote, hiyo inapaswa iwe ni wewe kuamini.

²³⁵ Vema, njoo, dada. Unaamini Mungu anaweza kuniruhusu nikuangalie huko nje, na kusema shida ya mwanamke huyu? Vema, waweza kuamini kwa moyo wako wote, dada, pia? Ungeamini? Vema, nenda na ugonjwa wako wa pumu utakuacha. Unaamini hilo? Vema. Nenda, ukamwamini Bwana Yesu kwa moyo wako wote.

²³⁶ Sasa, mwanamke huyu anayekuja hapa, unataka kujua ana shida gani? Ni ugonjwa wa tumbo. Nenda ukajipatie sambusa, Mungu anakuponya, anakupa afya. Amini.

Mungu anaweza kukufanyia yale Asthmador haitakufanyia. Unaamini hilo? Basi nenda zako ukishangilia.

Maskini kikohozi hicho, toka ndani yake, katika Jina la Yesu Kristo!

Mungu akubariki, nenda ukaamini.

²³⁷ Vipi kama ningekwambia, uliponywa ulipofika, kipandio cha juu, ungeamini neno langu kwa ajili yake? Nenda, ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana.” Nenda ukaponywe, amini kwa moyo wako wote.

²³⁸ Wewe ni mwanamke anayeonekana mwenye afya sana asiyeweza kusumbuliwa na mishipa, lakini hiyo ndiyo shida yako. Nenda, yote yamekwisha sasa. Unaona? Kukoma hedhi, hilo badiliko tu.

²³⁹ Sasa, unaamini huo ugonjwa wa pumu unakuacha, pia, ugonjwa wa akina mama na ugonjwa wa pumu? Nenda zako ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana. Ananiponya.”

²⁴⁰ Ni wangapi huko nje wanaotaka kumwamini Bwana Yesu Kristo? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba *huyu* ni Roho Mtakatifu, ya kwamba mimi ni ndugu yenu? Basi Roho Mtakatifu yuko hapa. Unaona mwanamke huyo ameponywa? Unaweza kuponywa, pia.

²⁴¹ Ni waaminio wangapi waliopo hapa? Inua mkono wako. Basi Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,

wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Wekeaneni mikono, wekeaneni mikono, ombeaneni.

²⁴² Bwana Yesu, njoo katika nguvu Zako. Ninakupa Wewe kusanyiko hili.

²⁴³ Shetani, umeshindwa vita. Toka kwenye kusanyiko hili, waache watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo!

²⁴⁴ Mungu aliye hai asifiwe! 

60-0722 Mlinzi, Habari Gani Za Usiku?
Lake County Fairgrounds
Lakeport, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org